# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA FEDHA




**KITABU CHA**
**WIZARA YA FEDHA NA TAASISI ZAKE**
**KUHUSU MIAKA (50) YA UHURU**
**WA TANZANIA BARA.**
**(1961 - 2011)**

# Hali ya Uongozi na Utawala kwa Wizara ya Fedha kutoka mwaka 1961 hadi hivi sasa.


Sir Ernest Vassey
1960 - 1961


Mh. Paul M. Bomani
1962 - 1965


Mh. Amir H. Jamal
1966- 1972, 1976- 1977, 1982.


Mh. Cleopa D Msuya
1974 - 1975, 1986- 1989



Mh. Edwin Mtei
1978- 1981.


Mh. Prof Kighoma A. Malima
1983-1985, 1993-1994



Mh. Stevene A. Kibona
1990- 1993


Mh. Jakaya M. Kikwete
1994-1995.


Mh. Prof. Simon M.Mbilinyi
1995-1996


Mh Daniel N. Yona
1997-2000


Mh. Basil P Mramba
2001-2005.


Mh Zakia H Meghji
2005-2007


Mh Mustapha H Mkulo
2008-Hadi sasa

**DIBAJI**

Tanzania Bara inasherehekea miaka 50 ya Uhuru ikushuhudia mafanikio na changamoto mbalimbali katika Uchumi na Huduma za Jamii. Wizara ya Fedha ni miongoni mwa Wizara zilizoanzishwa mara baada ya kupata Uhuru mwaka 1961.

Dira ya Wizara ya Fedha ni kuwa na Uchumi unaokua kwa kiwango cha juu na kupata matokeo yatakanufaisha wananchi wote.

Katika kuadhimisha miaka 50 ya uhuru tumeshuhudia mafaniikio mbalimbali yaliyopatikana katika nyanja za Uchumi na Huduma za Jamii kama vile kuongezeka kwa fursa za elimu, kuboreshwa kwa huduma za afya, upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wengi zaidi, kilimo cha kisasa na kuimarishwa kwa miundombinu ya barabara.

Pamoja na mafanikio hayo, Wizara ya Fedha imekabiliana na changamoto mbalimbali tangu Uhuru. Baadhi ya changamoto hizo ni juhudi za kuongeza mapato ya ndani yanayokidhi mahitaji ya nchi; Kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi; Kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana; Kuhakikisha maisha bora na ustawi wa jamii; na madhara yaliyosababishwa na mtikisiko wa uchumi duniani.

Katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza, Wizara ya Fedha imechukua hatua madhubuti ya Sera za mageuzi ya Kijamii na kiuchumi. Vilevile, mikakati mbalimbali imechukuliwa ya kuondoa umaskini na kukuza uchumi.

Wizara ya Fedha inamatarajio ya kuhakikisha kuwa Tanzania inafikia uchumi ulioimarika unaowezesha wananchi wake kushiriki kikamilifu katika kumiliki uchumi wa nchi. Pia, kuwa na vyanzo mbalimbali vya uzalishaji na uchumi wenye maendeleo ya viwanda ili kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi pamoja na kuwa na maisha bora na ustawi wa jamii wa kujitosheleza kwa chakula na kufikia usawa wa kijinsia.

## SHUKURANI

Kukamilika kwa Kitabu hiki cha Wizara ya Fedha na Taasisi zake kuhusu Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara kumetokana na jitihada zenye kuthaminika za Viongozi wa Wizara, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wafanyakazi na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizochini ya Wizara ya Fedha.

Shukurani za pekee zimwendee Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha kwa juhudi na jitihada zilizofanikisha uandaaji taarifa hii.

Mwisho, natoa shukurani za dhati kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha hatua za mwisho za kukamilika kwa taarifa hii.

Tumethubutu Tumeweza na Tunazidi kusonga mbele.

Mustafa H. Mkulo
WAZIRI WA FEDHA
Oktoba, 2011

## VIFUPISHO

| KIFUPI | MAANA |
|---|---|
| AGITF | Agricultural Inputs Trust Fund |
| ASDP | Agriculture Sector Development Programme |
| ATHCO | Air Tanzania Holding Corporation |
| BOT | Bank of Tanzania |
| BTC- | Belgium Technical Cooperation |
| BWM- | Benjamin William Mkapa |
| CGS | Commodity Guarantee Scheme |
| CHC | Consolidated Holding Corporation |
| CMSA | Capital Markets and Securities Authority |
| DSA | Dar es Salaam School of Accountancy |
| DSE | Dar es Salaam Stock Exchange |
| E- LEARNING | Electronic Learning |
| EAC | East Africa Cooperation |
| EADB | East African Development Bank |
| EASTC | East Africa Statistical Training Centre |
| ECGS | External Commodity Guarantee Scheme |
| EED | Economic Empowerment Department |
| EIB | European Investment Bank |
| EPZ | Export Processing Zone |
| EPZA | Export Processing Zone Authority |
| FIU | Financial Intelligence Unit |
| GBS | General Budget Support |
| GBT | Gaming Board of Tanzania |
| GDP | Gross Domestic Product |

| | |
|---|---|
| GEPF | Government Employees Provident Fund |
| GPSA | Government Procurement Service Agency |
| HIPC | Highly Indebted Poor Countries |
| IAA | Institute of Accountancy Arusha |
| IFM | Institute of Finance Management |
| IFMS | Intergrated Financial Management System |
| IMF | International Monetary Fund |
| IRDP | Institute of Rural Development Planning |
| IT | Information Technology |
| J.K | Jakaya Kikwete |
| JFC | Joint Finance Commission |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| KCMC | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| LART | Loans Advance Realizations Trust |
| LM | Logistic Management |
| MBA | Masters of Business Administration |
| MCA - T | Millennium Challenge Account -Tanzania |
| MCC | Millennium Challenge Cooperation |
| MEF | Mwananchi Empowerment Fund |
| MPAMITA | Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania |
| NBAA | National Board of Accountants and Auditors |
| NBC | National Bank of Commerce |
| NBMM | National Board of Materials Management |
| NBS | National Bureau of Statistics |
| NEDF | National Entrepreneurs Development Fund |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |


| | |
|---|---|
| NGO | Non Governmental Organization |
| NIC | National Insurance Corporation |
| PAC | Public Accounts Committee |
| PED | Poverty Eradication Department |
| PFMRP | Public Finance Management Reforms Programme |
| PMU | Procurement Management Unit |
| PPAA | Public Procurement Appeals Authority |
| PPRA | Public Procurement Regulatory Authority |
| PSPF | Public Service Pensions Fund |
| PSPTB | Procurement and Supplies Professionals and Technician's Board |
| PSRC | Public Service Reforms Commission |
| PTF | President Trust Fund |
| SACCOS | Savings and Community Cooperative Society |
| SADC | Southern Africa Development Cooperation |
| SELF | Small Entrepreneurs Loan Facility |
| SEZ | Special Economic Zone |
| SME | Small and Medium Enterprises |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TBCL | Twiga Bancorp Limited |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TIA | Tanzania Institute of Accountancy |
| TIB | Tanzania Investment Bank |
| TIRA | Tanzania Insurance Regulatory Authority |
| TOL | Tanzania Oxygen Limited |
| TPB | Tanzania Postal Bank |
| TR | Treasury Registrar |

| | |
|---|---|
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TRAB | Tax Revenue Appeals Board |
| TRAT | Tax Revenue Appeals Tribunal |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UTT | Unit Trust of Tanzania |
| VAT | Value Added Tax |
| WB | World Bank |
| YDF | Youth Development Fund |


**Yaliyomo** **Uk.**

| | |
|---|---|
| Dibaji | i |
| Shukurani | ii |
| Vifupisho | iii |
| Yaliyomo | vii |
| 1. Utangulizi | 1 |
| 2. Dira ya wizara | 1 |
| 3. Dhamira ya wizara | 2 |
| 4. Muundo na majukumu ya wizara kuanzia mwaka 1962 hadi sasa | 2 |
| 5. Majukumu ya wizara | 7 |
| 6. Hali ya uongozi na utawala kuanzia mwaka 1961 hadi sasa | 8 |
| 7. Majukumu ya jumla ya idara na vitengo | 13 |
| 8. Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya wizara ya fedha | 18 |
| 9. Sera na Sheria zilizokuwepo tangu uhuru hadi sasa | 53 |
| 10. Mabadiliko na Matukio makuu katika mfumo wa kiuchumi | 75 |
| 11. Mafanikio yaliyopatikana tangu wakati wa kupata uhuru hadi sasa 1961 - 2011 | 77 |
| 12. Changamoto zilizotitokeza tangu uhuru mwaka 1961 | 94 |
| 13. Matarajio ya Wizara ya Fedha katika miaka Hamsini 50 ljayo | 95 |


## Uongozi na Utawala wa Wizara ya Fedha wa sasa.




Mh. Mustafa H. Mkulo
Waziri wa Fedha




Mh. Pereira A. Silima (Mb)
Naibu Waziri wa Fedha.



Mh. Gregory G. Teu (Mb)
Naibu Waziri wa Fedha.



Ramadhani M. Khijjah
Katibu Mkuu.



Dkt. Servacius B. Likwelile
Naibu Katibu Mkuu.



Bi. Elizabeth J. Nyambibo
Naibu Katibu Mkuu.



Laston T. Msongole
Naibu Katibu Mkuu.

## 1.0 UTANGULIZI:

Tanzania Bara itasherehekea miaka hamsini 50 ya Uhuru huku ikishuhudia mafanikio na changamoto mbalimbali katika kipindi hicho. Wizara ya Fedha ni moja kati ya Wizara zilizoanzishwa mara baada ya kupata Uhuru mwaka 1961. Serikali ya Awamu ya Kwanza iliyoundwa baada ya kupata Uhuru ilianza kutekeleza majukumu yake mwaka 1962. Aidha, Hati ya Majukumu ilitolewa na kuainisha wajibu wa kila Wizara.

Kufuatia mabadiliko mbalimbali ya uongozi wa nchi yetu, Wizara ya Fedha nayo ilipitia mabadiliko hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamiaji wa shughuli za Serikali. Mabadiliko hayo yalilenga katika maeneo ya uongozi na majukumu na kusababisha jina la Wizara kubadilika mara kwa mara kwa lengo la kukidhi utekelezaji wa majukumu iliyopangiwa.

Tangu wakati wa kupata Uhuru hadi sasa Wizara imekuwa na majina tofauti ambayo ni Wizara ya Fedha (1962), Wizara ya Fedha na Mipango (1976), Wizara ya Nchi, Mipango na Uchumi (1983), Wizara ya Fedha na Uchumi (2008) na Wizara ya Fedha (2010). Mabadiliko haya yalienda sanjari na mabadiliko ya Muundo wa Wizara ili kuongeza ufanisi katika usimamiaji wa shughuli za Serikali.

## 2.0 DIRA YA WIZARA

Dira ya Wizara ya Fedha ni kuwa na Uchumi unaokua kwa kiwango cha juu na kupata matokeo yatakayonufaisha wananchi wote na kuhakikisha usimamizi thabiti wa fedha za Umma na uwajibikaji.

## 3.0 DHAMIRA YA WIZARA

Dhamira ya Wizara ni kuongeza kiwango cha ukuaji uchumi na kuhakikisha uchumi unaendelea kukua na kuendeleza uchumi tulivu kwa kubuni na kutekeleza Sera bora za uchumi na fedha, pamoja na kufanikisha uratibu na usimamizi wa rasilimali fedha, kuboresha na kuinua viwango vya taaluma na matumizi ya teknolojia ya habari.

## 4.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA KUANZIA MWAKA 1962 HADI SASA

Tangu kipindi cha mwaka 1962 hadi sasa, Muundo wa Wizara ya Fedha kwa nyakati tofauti umekuwa ukibadilika ili kuendana na mabadiliko ya Serikali. Utekelezaji wa shughuli za Wizara unazingatia jinsi majukumu yalivyoainishwa katika Hati ya Majukumu ya Serikali (Government Instrument) ambapo Hati ya kwanza ya majukumu ya Serikali ilitolewa mwaka 1962. Majukumu ya msingi yaliyokabidhiwa kutekelezwa chini ya Wizara ya Fedha mwaka 1962 ni kama ifuatavyo;

a. Kushughulikia makadirio ya Sera za Fedha na Uhasibu,
b. Ushuru na Forodha,
c. Utunzaji wa mali za adui (Custodian of enemy properties),
d. Maendeleo ya mipango (Bungeni),
e. Masuala ya Jumuia ya Madola, uhusiano wa kiuchumi na nchi za nje, masuala ya misaada kutoka nje,
f. Sera za fedha na Uchumi,
g. Udhibiti wa fedha, Kodi na Bima,
h. Uratibu wa taasisi za umma,
i. Masuala ya Posta na Benki,
j. Ngazi za mishahara,
k. Ushuru wa stempu,
l. Mapato,

m. Masuala ya takwimu na utafiti wa kiuchumi, na
n. Huduma za pamoja za Afrika Mashariki katika kamati za fedha.

Mwaka 1995, mara baada ya Uchaguzi ulioiingiza madarakani Serikali ya Awamu ya Tatu, majukumu ya Wizara yaliongezeka na mengine kuondolewa ili kukidhi utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa ufanisi. Katika Hati ya Majukumu iliyotolewa na Serikali, Wizara ya Fedha ilikabidhiwa dhamana ya kutekeleza majukumu yafuatayo;

a. Udhibiti na usimamaizi wa sera za fedha,
b. Masuala ya kodi, mapato, huduma za mapato ya ndani,
c. Bajeti ya Serikali,
d. Masuala ya ushuru na forodha,
e. Sera za Mikopo,
f. Misaada ya Fedha kutoka nje,
g. Masuala ya uhusiano kati ya taasisi za fedha za kimataifa; IMF, WB, EADB, ACP/EEC/EIB,
h. Udhibiti na usimamizi wa thamani ya fedha na viwango vya ubadilishaji wa fedha,
i. Sera za uhasibu,
j. Usimamizi wa mali za Serikali,
k. Ushuru wa stempu,
l. Kutunza mali za adui (Custodian of enermy properties),
m. Udhibiti wa uingizaji wa bidhaa kutoka nje,
n. Kusimamia deni la Taifa,
o. Uendelezaji wa rasilimali watu,
p. Masuala ya fedha ya Jumuiya ya Madola,
q. Kusimamia taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mapato na daftari kuu la usajili wa magari ya Serikali, na
r. Kusimamia Mashirika ya Umma na Idara zinazojitegemea.

Kutoka mwaka 1995 ilipotolewa hati ya majukumu, Wizara ya Fedha haikuwa na mabadiliko makubwa ya kimuundo hadi mwezi Februari, 2008 baada ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuunganisha Wizara mbili zilizokuwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Katika hatua hii jina la Wizara lilibadilika na kuitwa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mabadiliko makubwa yaliyotokana na kuunganishwa kwa Wizara hizi mbili ni kuhamishiwa kwa Idara mbili zilizokuwa chini ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Idara hizi ni pamoja na Idara ya Kuondoa Umaskini (PED) na ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (EED) ambazo zilizounganishwa na kuunda Idara ya Kuondoa Umaskini na Uwezeshaji Kiuchumi.

Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Wizara ilikuwa ikitekeleza majukumu yake ya msingi kama ilivyokuwa imepangiwa. Kufuatia Uchaguzi huo, majukumu ya Wizara yalibadilika kutokana na kuhamishwa kwa shughuli zingine zilizokuwa chini ya Wizara hii. Katika mabadiliko hayo, shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi zilihamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na za masuala ya uchumi zilipelekwa Tume ya Mipango kama msimamizi mkuu na Wizara ya Fedha kuwa mchangiaji katika kutekeleza jukumu hilo. Pia, Wizara iliongezewa jukumu la kushughulikia masuala ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi pamoja na masuala ya maendeleo ya tija nchini.

## JEDWALI NA. 1

Linaonyesha Idadi ya Idara na Vitengo vilivyopo Wizara ya Fedha kulingana na muundo

| Na | Idara/Kitengo |
|---|---|
| 1 | Idara ya Uchambuzi wa Sera |
| 2 | Idara ya Fedha za Nje |
| 3 | Idara ya Kuondoa Umaskini |
| 4 | Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali |
| 5 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali |
| 6 | Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali |
| 7 | Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Fedha |
| 8 | Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali |
| 9 | Idara ya Mipango |
| 10 | Idara ya Utawala na Rasilimali Watu |
| 11 | Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma |
| 12 | Kitengo cha Sheria |
| 13 | Kitengo cha Mawasiliano Serikalini |
| 14 | Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani |
| 15 | Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 16 | Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi |
| 17 | Kitengo cha Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi |
| 18 | Kitengo cha Uratibu na Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA |

**JEDWALI NA. 2**

Linaonyesha idadi ya Taasisi ambazo zipo chini ya Wizara ya Fedha:-

| Na. | Jina la Taasisi/Shirika |
|---|---|
| 1 | Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR) |
| 2 | Benki Kuu ya Tanzania (BOT) |
| 3 | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) |
| 4 | Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) |
| 5 | Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) |
| 6 | Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) |
| 7 | Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali (GEPF) |
| 8 | Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) |
| 9 | Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) |
| 10 | Mfuko wa Pensheni wa PPF |
| 11 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) |
| 12 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) |
| 13 | Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) |
| 14 | Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki (EASTC) |
| 15 | Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) |
| 16 | Kitengo cha Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu (FIU) |
| 17 | Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) |
| 18 | Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) |
| 19 | Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (PPAA) |
| 20 | Tume ya Fedha ya Pamoja (JFC) |
| 21 | Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) |
| 22 | Benki ya Posta Tanzania (TPB) |
| 23 | Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) |
| 24 | Twiga Bancorp Limited (TBCL) |
| 25 | Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) |

| | |
|---|---|
| 26 | Shirika Hodhi la Serikali (CHC) |
| 27 | Shirika la Bima la Taifa (NIC) |
| 28 | Mfuko wa Changamoto za Milenia Tanzania (MCA - T) |
| 29 | Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) |
| 30 | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) |
| 31 | Wakala Wa Ununuzi Serikalini (GPSA) |
| 32 | Mfuko wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo(SELF) |

## 5.0 MAJUKUMU YA WIZARA

a. Kusimamia utekelezaji wa Sera za uchumi jumla,
b. Kusimamia uwajibikaji kwenye usimamizi wa fedha na mapato ya Serikali,
c. Kuendeleza mawasiliano na kushirikisha wadau katika uandaaji wa Sera za Fedha,
d. Usimamizi na udhibiti wa bajeti ya Serikali,
e. Kufuatilia, kuratibu na kudhibiti rasilimali kutoka nje na ndani ya nchi,
f. Kusimamia na kudhibiti usimamizi wa mali na vifaa vya Serikali,
g. Kusimamia na kuratibu mfumo wa taarifa za kiuhasibu Serikalini,
h. Kusimamia na kudhibiti deni la Taifa,
i. Kusimamia na kudhibiti misaada na mikopo,
j. Kusimamia vitegauchumi vya Serikali katika kampuni mbalimbali na Mashirika ya Umma,
k. Kukagua na kuhakikisha thamani ya matumizi ya Fedha za Serikali kulingana na mafungu yaliyogawiwa,
l. Kusimamia masuala ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

## 6.0 HALI YA UONGOZI NA UTAWALA KUANZIA MWAKA 1961 HADI SASA

Kutoka mwaka 1962 ilipoundwa Serikali ya awamu ya kwanza mara baada ya kupata uhuru hadi sasa, Wizara ya Fedha imeongozwa na Mawaziri 12 katika vipindi tofauti na Manaibu Waziri zaidi ya 10. Kama ilivyo sasa, uteuzi wa Manaibu Waziri ulizingatia uwakilishi kutoka pande zote za Muungano wa nchi yetu. Kwa nyakati tofauti, Wizara ya Fedha imewahi pia kuongozwa na Waziri bila kuwa na Naibu Waziri. Ufuatao ni muhtasari wa taarifa ya hali ya uongozi kutoka mwaka 1962 hadi sasa. (Jedwali Na. 3 kwa ajili ya rejea)

**JEDWALI NA. 3**

Linaonyesha Mawaziri na Naibu Mawaziri walioongoza Wizara ya Fedha.

| Na. | Mwaka | Waziri | Naibu Waziri |
|---|---|---|---|
| 1. | 1959-1961 | Sir. Ernest Vassey | Wazi |
| 2. | 1962-1965 | Paul M. Bomani | F.B. Mponji |
| 3. | 1966- 1972 | Amir H. Jamal | S. S. Rashid |
| 4. | 1974- 1975 | Cleopa D. Msuya | Juma H. Omary |
| 5. | 1976- 1977 | Amir H. Jamal | Venance F. Ngula |
| 6. | 1978- 1981 | Edwin Mtei | Venance F. Ngula |
| 7. | 1982 | Amir H. Jamal | Venance F. Ngula |
| 8. | 1983-1985 | Prof. Kighoma A. Malima | S.A.Kibona Arcado D. Ntagazwa |
| 9. | 1986- 1989 | Cleopa D. Msuya | 1. Amina S. Ally<br>2. Juma H. Omary |
| 10. | 1990- 1993 | Steven A. Kibona | Juma H. Omary |
| 11. | 1993-1994 | Prof. Kighoma A. Malima | Simai P. Makame |
| 12. | 1994-1995 | Jakaya M. Kikwete | Simai P. Makame |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | 1995-1996 | Prof. Simon M. Mbilinyi | Kilontsi M. Mporogomyi |
| 14. | 1997-2000 | Daniel N. Yona | 1. Abdisalaam I. hatibu<br>2. Monica N. Mbega |
| 15. | 2001-2005 | Basil P. Mramba | 1. Dr. Festus Limbu<br>2. Abdisalaam I. Khatibu |
| 16. | 2005-2007 | Zakia H. Meghji | 1. Abdisalaam I. Khatibu<br>2. Mustapha H. Mkulo |
| 17. | 2008-2010 | Mustafa H. Mkulo | 1. Omary Y. Mzee<br>2. Jeremiah Sumari |
| 18. | 2010 - sasa | Mustafa H. Mkulo | 1. Gregory G. Teu<br>2. Pereira A. Silima |

## JEDWALI NA. 4

Linaonyesha viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara ya Fedha wanaoongoza Idara na Vitengo vya Wizara kwa sasa.

| Na. | Jina | Cheo |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Mustafa H. Mkulo | Waziri (Mb) |
| 2 | Mhe. Gregory G. Teu | Naibu Waziri (Mb) |
| 3 | Mhe. Pereira A. Silima | Naibu Waziri (Mb) |
| 4 | Bw. Ramadhani M. Khijjah | Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali |
| 5 | Bi. Elizabeth J. Nyambibo | Naibu Katibu Mkuu |
| 6 | Bw. Laston T. Msongole | Naibu Katibu Mkuu |
| 7 | Dkt. Servacius B. Likwelile | Naibu Katibu Mkuu |
| 8 | Bi. Donesia R. Makani | Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu |
| 9 | Bw. Bedason A. Shallanda | Kamishna wa Sera |
| 10 | Bw. Shogholo C. Msangi | Kamishna Msaidizi wa Sera |
| 11 | Dkt. Yamungu Kayandabila | Kamishna Msaidizi wa Sera |
| 12 | Bw. Sephania Mwakipesile | Kamishna Msaidizi wa Sera |
| 13 | Bw. Augustine Olall | Kamishna Msaidizi wa Sera |
| 14 | Bw. Charles Samanyi | Kamishna Msaidizi wa Sera |

| | | |
|---|---|---|
| 15 | Bw. Peter M. Mshangila | Kaimu Mkurugenzi wa Mifumo ya Fedha |
| 16 | Bi. Zubeda Mahugu | Mkurugenzi Msaidizi wa Mifumo ya Fedha |
| 17 | Bw. Hamza Rashid | Mkurugenzi Msaidizi wa MIfumo ya Fedha |
| 18 | Bw. Ezra M. I. Msanya | Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za Serikali |
| 19 | Bi. Herith E. Chamuriho | Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Mali za Serikali |
| 20 | Bw. Sixbert H. Qamdiye | Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Mali za Serikali |
| 21 | Bi. Monica Mwamunyange | Kamishna wa Bajeti |
| 22 | Bw. Ramadhan Hamis | Kamishna Msaidizi wa Bajeti |
| 23 | Bw. Pius M. Mponzi | Kamishna Msaidizi wa Bajeti |
| 24 | Bw. John W. Mwilima | Kamishna Msaidizi wa Bajeti |
| 25 | Bi. Edna N. Nyanguli | Kamishna Msaidizi wa Bajeti |
| 26 | Bw. John Cheyo | Kamishna Msaidizi wa Bajeti |
| 27 | Bw. Ngosha S. Magonya | Kamishna wa Fedha za Nje |
| 28 | Bw. Jerome J. Buretta | Kamishna Msaidizi wa Fedha za Nje |
| 29 | Bi. Philipina W. Malisa | Kamishna Msaidizi wa Fedha za Nje |
| 30 | Bi. Mameltha K. Mutagwaba | Kamishna Msaidizi wa Fedha za Nje |
| 31 | Bi. Judica Omari | Kaimu Kamishna Msaidizi wa Fedha za Nje |
| 32 | Dkt. Fredrick Mwakibinga | Mkurugenzi wa Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma |
| 33 | Bi. Fatima S. Kiongosya | Mkurugenzi wa Idara ya Mipango |
| 34 | Bi. Mwanaidi M. Mtanda | Mhasibu Mkuu wa Serikali |
| 35 | Bw. Mohamed A. Mtonga | Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali |
| 36 | Bw. Constantine Mashoko | Mkaguzi Mkuu Msaidizi wa Ndani wa Serikali |
| 37 | Bw. Amin Mcharo | Mkaguzi Mkuu Msaidizi wa Ndani wa Serikali |
| 38 | Stanslaus Mpembe | Mkaguzi Mkuu Msaidizi wa Ndani wa Serikali |
| 39 | Choto L. Sendo | Mkaguzi Mkuu Msaidizi wa Ndani wa Serikali |
| 40 | Emmanuel M. Subbi | Mkaguzi Mkuu Msaidizi wa Ndani wa Serikali |
| 41 | Bw. Eliakim Lovililo | Mhasibu Mkuu Msaidizi wa Serikali |
| 42 | Bw. Ishmael Kasekwa | Mhasibu Mkuu Msaidizi wa Serikali |
| 43 | Bw. Aziz H. Kifile | Mhasibu Mkuu Msaidizi wa Serikali |

| | | |
|---|---|---|
| 44 | Bi. Irene Kasambala | Mhasibu Mkuu Msaidizi wa Serikali |
| 45 | Bw. Victus Paul | Mhasibu Mkuu Msaidizi wa Serikali |
| 46 | Bi. Veronica U. Lyapa | Mhasibu Mkuu wa Wizara (Fungu 50) |
| 47 | Bw. Sayi Nsungi | Mhasibu Mkuu wa Wizara (Fungu 21) |
| 48 | Bi. Susana B. Mkapa | Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria |
| 49 | Bw. Idd T. Lemmah | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi |
| 50 | Bi. Ingiahedi C. Mduma | Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini |
| 51 | Bi. Anna Mwasha | Mkurugenzi wa Idara ya Kuondoa Umaskini |
| 52 | Bw. Victor P. Mwainyekule | Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kuondoa Umaskini |
| 53 | Bw. Servus A. Sagday | Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kuondoa Umaskini |
| 54 | Dkt. Frank Mhilu | Kaimu kamishna wa Kitengo cha Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi |

**JEDWALI NA. 5**

Linaonyesha viongozi na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizochini ya Wizara:

| Na. | Jina | Cheo |
|---|---|---|
| 1 | Bw. Geofrey K. Msella | Kaimu Msajili wa Hazina – TR |
| 2 | Prof. Benno Ndulu | Gavana – BoT |
| 3 | Bw. Harry M. Kitilya | Kamishna Mkuu - TRA |
| 4 | Bw. Adam Maingu | Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa - PSPF |
| 5 | Bw. Daudi Msangi | Mkurugenzi Mkuu wa - GEPF |
| 6 | Dkt. Hamis S. Kibola | Mtendaji Mkuu - UTT |
| 7 | Bw. Justin P. Mwandu | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji - NIC |
| 8 | Bw. Peter M. Noni | Mtendaji Mkuu - TIB |
| 9 | Dkt. Fratern M. Mboya | Mtendaji Mkuu - CMSA |
| 10 | Bw. Pius A. Maneno | Mkurugenzi Mtendaji - NBAA |
| 11 | Bw. Sabasaba K. Moshingi | Mtendaji Mkuu - TPB |
| 12 | Dkt. Ramadhani S. Mlinga | Mtendaji Mkuu – PPRA |
| 13 | Bw. Israel Kamuzora | Kamishna wa Bima - TIRA |

kusaidia Bajeti ya Serikali. Majukumu mengine ya Idara ni pamoja na kutekeleza Mkakati wa Pamoja wa Misaada

Tanzania (MPAMITA) kwa kuzingatia makubaliano ya kimataifa kuhusu ufanisi wa misaada.

### 7.4 Idara ya Kuondoa Umaskini

Idara ya Kuondoa Umaskini ina jukumu la Kuratibu uandaaji, na kusimamia utekelezaji wa Sera na mikakati ya kuondoa umaskini. Idara pia inaratibu utekelezaji wa programu mbalimbali za kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

### 7.5 Idara ya Usimamizi wa Bajeti

Jukumu kuu la Idara ni kutoa huduma na utaalam juu ya Bajeti ya Serikali, kugawa rasilimali fedha zilizoidhinishwa, kufuatilia matumizi ya Umma pamoja na kuboresha mifumo ya bajeti.

### 7.6 Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Fedha

Majukumu ya msingi ya Idara hii ni kutoa taarifa za malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali kila mwezi na kuhudumia miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Idara zote za Wizara.

### 7.7 Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali

Jukumu kuu la Idara ni kubuni na kusimamia sera, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia udhibiti, utunzaji, utumiaji na uondoshaji wa mali za Serikali ili kuhakikisha Serikali inapata thamani bora ya pesa zake.

### 7.8 Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali

Jukumu la Idara ni kusimamia, kufuatilia, kushauri na kudhibiti matumizi ya Fedha za Umma katika Wizara, Idara zinazojitegemea na katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 7.9 Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma

Idara hii ina majukumu ya kuandaa na kusimamia Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma, kupitia sera, sheria, kanuni na miongozo mingine ya ununuzi wa umma kwa lengo la kufanyia marekebisho na kufanya tathimini ya utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.

### 7.10 Idara ya Mipango

Jukumu Kuu la Idara hii ni kupanga, kuandaa bajeti ya wizara na ufuatiliaji wa tathmini ya programu na miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Fedha. Aidha, majukumu mengine ni pamoja na kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa wizara wa muda wa kati na kuratibu shughuli za wizara bungeni.

### 7.11 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

Idara hii inasimamia usimamizi wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 Sura Na. 34; Utayarishaji na usimamizi wa Hesabu za Serikali; Utayarishaji na usimamizi wa Sera za Serikali zinazohusu ubora na usalama wa fedha na mali zote za Serikali; Utoaji wa miongozo, ikiwa ni pamoja na ile ya kiujumla au inayolenga maeneo fulani kwa Maofisa Wahasibu kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2001.

Aidha, majukumu mengine ni pamoja na kuandaa na kusimamia malipo yote ya Serikali; Kuandaa malipo ya pensheni; Kusimamia na kuratibu masuala yote ya usimamizi wa fedha katika Serikali; na kutayarisha majumuisho ya Hesabu za Serikali.

## 7.12 Kitengo cha Sheria

Kitengo cha Sheria kinaratibu masuala yote ya kisheria yanayohusu Wizara ya Fedha na Taasisi zake. Baadhi ya majukumu muhimu ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kuhusu masuala mbalimbali kwa Idara na Vitengo vilivyochini ya wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Kuandaa nyaraka mbalimbali za kisheria ikiwemo mikataba pamoja na Hati mbalimbali zinazohusu Wizara ya Fedha; Kuratibu maandalizi ya Miswada ya Sheria mbalimbali za fedha ikiwa ni pamoja na Muswada wa Fedha; na kuratibu shughuli za Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu.

## 7.13 Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Majukumu ya kitengo hiki ni kutayarisha, kuchapisha na kusambaza majarida, vipeperushi, makala na taarifa mbalimbali zinazohusu wizara kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi kuhusu mafanikio ya wizara, kuelezea sera, programu na kazi zinazofanywa na wizara; Kutayarisha na kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara; Kuratibu uandaaji wa makala za kisekta na kiwizara kwa ajili ya warsha, semina na mikutano; Kuratibu uandaaji, utoaji na usambazaji wa makala ya kisekta na wizara; Kutoa elimu kwa umma kupitia magazeti, redio na luninga pia ushiriki wa wizara katika maonyesho ya Utumishi wa umma, Saba Saba na Nane Nane; Kuhuisha tovuti ya Wizara ya Fedha

(www.mof.go.tz); Kutoa ushauri katika Idara, Vitengo, Idara nyingine za wizara, wakala tendaji na Asasi zisizo za kibiashara kuhusu masuala yote ya mawasiliano na utoaji wa nyaraka mbalimbali kwa wadau; Kujibu hoja na kutolea ufafanuzi, malalamiko na kero mbalimbali zinazotolewa na wananchi, kupitia vyombo vya habari.

## 7.14 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Majukumu ya kitengo hiki ni kukagua na kutoa taarifa kuhusu mapokezi, utunzaji wa fedha na matumizi ya mali za Serikali, kukagua na kutoa taarifa kuhusu utekekezaji wa kanuni za fedha kama zilivyoainishwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali, kukagua na kutoa taarifa ya utaratibu uliopo kuhusu utunzaji bora wa mali za Serikali na kuhakiki na kutoa taarifa juu ya ubora wa vidhibiti vilivyopo kwenye mtandao wa Kompyuta.

## 7.15 Kitengo cha Fedha na Uhasibu

Majukumu ya msingi ya kitengo ni kusimamia, kudhibiti na kutoa ushauri wa kihasibu na fedha katika fungu husika; Kuandaa taarifa za hesabu za Wizara za mwaka; Kuandaa taarifa za utekelezaji, maduhuli na matumizi kwa vipindi tofauti ikiwa ni robo, nusu na mwaka mzima; Kuratibu maandalizi ya bajeti, bajeti ya maduhuli, mishahara na matumizi mengineyo; na kuratibu maandalizi ya kikao cha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kinachojadili hesabu za mwaka za fungu husika na kufuatilia taarifa za utekelezaji wa maagizo ya Kamati hiyo.

### 7.16 Kitengo cha Menejimenti ya Ununuzi (PMU)

Majukumu ya Kitengo hiki ni kusimamia na kuhakikisha upatikanaji wa huduma na vifaa mbalimbali kwa Idara na vitengo vyote vya Wizara; Kuandaa Mpango wa Ununuzi wa Wizara pamoja na uondoshwaji wa vifaa chakavu; na kutoa ushauri wa kitalaam kuhusu masuala ya ununuzi na kutunza kumbukumbu zote za ununuzi wa vifaa na huduma mbalimbali.

### 7.17 Kitengo cha Usimamizi na Uratibu wa Mifumo ya TEHAMA

Kitengo hiki kinashughulika na masuala ya TEHAMA katika Idara na Vitengo vya Wizara.

### 7.18 Kitengo cha Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi

Majukumu ya msingi ya Kitengo ni pamoja na kutathmini, kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya shughuli na miradi inayosimamiwa chini ya mfumo wa Ubia .

## 8.0 TAASISI NA MASHIRIKA YALIYO CHINI YA WIZARA YA FEDHA

### 8.1 Ofisi ya Msajili wa Hazina – TR

Ofisi ya Msajili wa Hazina imeundwa kwa Sheria Na. 35 Sura Na. 418 ya mwaka 1959. Sheria hiyo imefanyiwa marekebisho makubwa mwaka 2002 na kuwa Treasury Registrar (Powers and Functions) Act. Cap. 370, na marekebisho mengine yalifanyika mwaka 2010 kupitia Sheria Na.11 ya mwaka 2010 na kuifanya iwe Ofisi ya kujitegemea.

Madhumuni ya kuundwa kwa Ofisi ni kutunza na kusimamia rasilimali za Serikali katika Mashirika na Asasi za Umma.

Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ni kuishauri Serikali kuundwa kwa Taasisi au Shirika la Umma; Kununua, kushikilia na kuuza rasilimali na mitaji ya Umma; Kufanya tathmini na kudhibiti utendaji kazi wa Mashirika na Taasisi za Umma; na kuitisha gawio na michango kutoka Mashirika ya Umma ambayo Serikali imewekeza hisa.

Katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeweza kuchambua na kuidhinisha bajeti za Mashirika na taasisi; Kusimamia mapato na matumizi kwa kuchambua Taarifa za robo na mwaka; Kukusanya gawio na michango inayoingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali; Kukusanya madeni na riba kwa mikopo iliyotolewa kwa Mashirika na Taasisi; na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya uanzishaji, uunganishaji na uvunjaji wa Mashirika ya Umma.

Ofisi ya Msajili wa Hazina inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mashirika na Taasisi za Umma kutochangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kama Sheria ya Fedha ya mwaka 2008 na Waraka wa Hazina Na.8 wa mwaka 2008/09 unavyotaka; Kuongezeka kwa madeni yatokanayo na mikopo iliyotolewa kwa njia ya dhamana ya Serikali kwa Mashirika au Taasisi mbalimbali; Uwezo mdogo wa Serikali kukidhi mahitaji makubwa ya mitaji kwa baadhi ya Mashirika ya Umma umeathiri utendaji wa Mashirika hayo kwa kiasi kikubwa. Pia Serikali kutokuwa na uwezo wa kutoa michango ya mitaji kwa Mashirika ambayo bado inaubia, kimeathiri ufanisi wa Mashirika hayo na wakati mwingine kuhatarisha hisa za Serikali katika Mashirika hayo kupungua thamani; na mikataba ya hiari inayofanywa kati ya menejimenti za Mashirika na wafanyakazi imekuwa

kiini cha migogoro katika Mashirika ya Umma pale shirika linaposhindwa kutekeleza makubaliano ya mkataba husika. Matokeo yake mwajiri anaposhindwa kutekeleza makubaliano hayo, wafanyakazi hurudi kwa Msajili wa Hazina kutaka walipwe madai yao kwa mujibu wa mkataba wa hiari.

## 8.2 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

### Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali Kuu – PSPF

Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali Kuu ni taasisi iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 2 ya Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 Sura Na. 371.

Baadhi ya majukumu ya Mfuko ni kutambua na kuandikisha Wanachama wa Mfuko; Kukusanya Michango ya pensheni kutoka kwa wafanyakazi wa Serikali na Wakala zake; Kutunza kumbukumbu za Utumishi wa Wanachama na za Wastaafu; Kuwekeza michango na mapato ya ziada yatokanayo na uwekezaji katika miradi mbalimbali; na ulipaji wa Mafao.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Mfuko huu ni pamoja na uboreshaji wa viwango vya malipo ya kiinua mgongo na pensheni ya kila mwezi; Mfuko unahifadhi kumbukumbu za wanachama kwa kutumia mfumo wa kisasa wa kompyuta; Mfuko umeweka utaratibu wa kuwakopesha wanachama wake nusu ya kiinua mgongo ili kuwawezesha kununua, kujenga au kukarabati nyumba. Mpango huu unawanufaisha wanachama ambao wamebakiza angalau miaka mitano kufikia umri wa kustaafu kwa lazima.

Sanjari na hilo, Mfuko unajenga nyumba za gharama nafuu katika mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya wanachama wake na jamii kwa ujumla; Kujenga jengo jipya la Bunge kwa kushirikiana na Serikali na mashirika mengine ya Hifadhi ya Jamii. Vilevile, Mfuko umejenga jengo la Chuo cha Elimu katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha Sayansi na Teknologia cha Nelson Mandela Afrika, umefadhili ujenzi wa nyumba za polisi zilizopo barabara ya Kilwa – Dar es Salaam, unajenga nyumba na kujenga jengo lake la ghorofa 23 lililopo Dar es Salaam; na mfuko umefanikiwa kufungua Ofisi katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Matarajio ya baadaye ya mfuko ni kuendelea kuboresha mafao ikiwemo pensheni ya kila mwezi kwa wanachama; Kuendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kutoka mikoa mitano ya sasa (Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Tabora na Mtwara) na kwenda nchi nzima ili kuwawezesha wanachama wake na wananchi kwa ujumla kuwa na makazi bora kwa bei nafuu; na kutafuta maeneo mapya ya uwekezaji ili kupata faida zaidi na hivyo kuimarisha uwezo wa Mfuko kulipa mafao mazuri zaidi.

**Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini – GEPF**

Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini (GEPF) ulianzishwa chini ya Sheria Na. 51 ya mwaka 1942, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Madhumuni ya Mfuko ni kutoa huduma ya hifadhi ya jamii katika mfumo wa akiba kwa watumishi wa Serikali Kuu walioajiriwa katika masharti ya mikataba, masharti ya kawaida na wengine wote ambao hawapati stahili ya pensheni.

Baadhi ya majukumu ya Mfuko ni kusajili wanachama; Kukusanya michango ya wanachama; Kuwekeza michango ya wanachama; na kulipa mafao kwa wanachama.

Mafanikio ya Mfuko yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwake mpaka sasa ni kuongezeka kwa idadi ya wanachama kutoka wanachama 16,131 mwaka 2004 mpaka wanachama 40,133 mwaka 2010; Michango imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 4.41 (2004) mpaka Shilingi bilioni 16.32 (2010) na mapato yatokanayo na uwekezaji yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 2.10 (2004) mpaka shilingi bilioni 7.70 (2010); Thamani ya Mfuko imeongezeka kufikia Shilingi bilioni 100.03; Mfuko umejitahidi kuboresha huduma kwa wanachama katika maeneo mbalimbali ikiwemo siku za kukokotoa mafao ya wanachama kushuka kutoka siku 14 mpaka siku 7 za kazi; na upatikanaji wa taarifa za wanachama ni rahisi wakati wowote mwanachama anapohitaji. Wanachama wanaweza kupata taarifa zao za michango kupitia tovuti ya Mfuko.

Matarajio ya baadaye ya Mfuko huo ni pamoja na kupanua wigo wa wanachama ili kila Mtanzania mzalishaji aweze kujiwekea akiba ya uzeeni; Mfuko kupitia skimu mpya ya kuchangia kwa hiari kwa wanachama wa sekta isiyo rasmi unafanya stadi ambayo itawezesha ongezeko la mafao yenye manufaa zaidi kwa wanachama wa skimu hii. Aidha, Mfuko unaangalia uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa kutoa mafao ya muda mrefu.

## Mfuko wa Pensheni wa PPF

Mfuko wa pensheni wa PPF ulianzishwa mwezi Julai 1978 chini ya Sheria Na. 14 ambayo kwa sasa inajulikana kama "Sheria ya Pensheni ya Mashirika ya Umma Sura Na. 372 kwa madhumuni ya kutoa mafao ya uzeeni na mafao ya aina nyingine kwa wanachama wa Mfuko huu.

Baadhi ya majukumu ya Mfuko ni kuandikisha wanachama; Kukusanya michango; Kuwekeza michango iliyokusanywa, na kulipa mafao.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukua kwa mtaji wa Mfuko kutoka shilingi bilioni 264.4 (2005) hadi kufikia shilingi bilioni 722.5 (2010); Pensheni ya kila mwezi hulipwa kwa wakati; Mfuko umeongeza kima cha chini cha pensheni hadi kufikia shilingi 50,000 kila mwezi. Aidha, tangu mwezi Mei 2010 wastaafu ambao walikuwa wakipokea kima cha chini cha pensheni cha zaidi ya Shilingi 50,000 kwa mwezi, Mfuko umeongeza asilimia 2 ya Pensheni yao. Wanachama wana uwezo wa kupata huduma za Mfuko kwa kutumia mtandao wa kompyuta au simu za mkononi; na huduma za wateja zimesogezwa karibu na wananchi kupitia kanda saba ambazo ni Kanda ya Ilala, Kanda ya Temeke, Kinondoni, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Mashariki na Kati, na Kanda ya Kaskazini. Pia huduma hizo zinapatikana katika Ofisi ndogo za Mfuko ambazo ziko Mafinga, Dodoma, na Kahama. Hii kwa kiasi kikubwa imerahisisha uandikishaji wa wanachama na huduma kwa ujumla.

Changamoto zilizojitokeza tangu kuanzishwa kwa Mfuko ni pamoja na kushuka kwa hali ya uchumi kutokana na mtikisiko wa masoko ya Fedha ulioikumba dunia mwishoni mwa mwaka 2008. Athari za mtikisiko huo ni pamoja na kufungwa kwa baadhi ya migodi ambako Mfuko ulikuwa na wanachama, kupunguzwa kwa wafanyakazi katika migodi iliyobaki na kutofunguliwa kwa migodi mipya; Ukwepaji wa uandikishaji wa wanachama katika Mfuko; Baadhi ya wanachama wamekuwa wanadai kulipwa mafao yao kutokana na kubadilika kwa mwajiri wakati mwanachama husika anaendelea na ajira; Baadhi ya waajiri kutowasilisha michango ya wanachama kwa

wakati na hivyo kusababisha usumbufu kwa wanachama wanapotakiwa kulipwa mafao yao kwa mujibu wa sheria.

Kutokana na kuwepo kwa Sheria mpya ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, Mfuko unatarajia kuongeza idadi ya wanachama wake kwa kusajili zaidi katika sekta binafsi na isiyo rasmi; Kuwekeza fedha za wanachama kwa kuzingatia vigezo bora; na kuongeza juhudi katika masuala ya utafiti hususan katika uboreshaji wa mafao kwa wanachama na kudhibiti matumizi yake kutoka asilimia 14 kwa mwaka 2008 hadi asilimia 10 mwaka 2012 kwa kutumia kigezo cha uwiano wa gharama za uendeshaji na michango.

## 8.3 Huduma za Kibenki

### Benki Kuu ya Tanzania – BoT

Benki Kuu ya Tanzania ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1965. Lengo lake kuu ni kuandaa, kusimamia na kutekeleza sera ya fedha yenye kuhakikisha utulivu wa bei za ndani kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi. Aidha, Benki Kuu ina jukumu la kuchapisha fedha, kuzisambaza na kuhakikisha kuna ujazi wa fedha wa kutosha nchini; Kutunza akiba ya taifa ya fedha za kigeni pia ni benki ya Serikali na msimamizi wa benki zote zilizopo nchini; Kutoa leseni kwa Benki na Taasisi zote za fedha hapa nchini; na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya masuala mbalimbali yanayohusu uchumi na maendeleo.

Ili kuweza kutimiza majukumu yake, Benki Kuu inazingatia mambo yafuatayo: Ongezeko la ujazi wa fedha unaokubalika, kasi ya ukuaji wa mikopo inayotolewa na Benki zingine na inayoendana na mahitaji halisi ya uzalishaji na malengo ya ujazi wa fedha, uwepo wa riba inayotegemea nguvu ya soko, uwepo wa akiba ya fedha

za kigeni inayotosheleza mahitaji ya nchi, Utulivu wa thamani ya Shilingi ikilinganishwa na sarafu kubwa duniani, kulinda na kuendeleza utulivu wa mabenki na taasisi za fedha nchini na uwepo wa masoko ya fedha yaliyoimara pamoja na mfumo madhubuti wa malipo.

Tangu kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania mwaka 1966, Sera ya Fedha nchini imekuwa ikibadilika mara kwa mara. Kwa mfano kati ya miaka ya 1960 hadi 1970, Sera ya Fedha ya Benki Kuu ilitegemea maelekezo kutoka Serikalini kupitia miongozo ya fedha na mikopo na ile ya fedha za kigeni iliyoanzishwa mwaka wa 1971/72.

Kuanzia mwaka 1993, Benki Kuu imekuwa ikihakikisha kunakuwepo na ujazi wa fedha katika kutekeleza Sera ya Fedha sanjari na hali halisi ya ukuaji wa masoko ya fedha na upatikanaji wa takwimu za kiuchumi. Mfumo huu unalenga katika kuhakikisha uwepo wa ujazi wa fedha unaoendana na ukuaji wa uchumi na pia utakaowezesha uwepo wa mfumuko wa bei wa chini na uliotulia. Benki Kuu huweka malengo yake ya mwaka ya ujazi wa fedha ambayo huchapishwa kama tamko la sera ya fedha na kuwasilishwa kwa Waziri wa Fedha na hatimaye kuwasilishwa bungeni. Malengo hayo hufanyiwa mapitio kila baada ya miezi sita kuhakikisha kwamba yako sanjari na malengo yaliyokusudiwa.

Mafanikio kadhaa yamepatikana katika utekelezaji wa Sera ya Fedha hasa katika kipindi cha miaka ya 1995 hadi 2010. Kwa mfano, mfumko wa bei ulishuka kutoka wastani wa asilimia 30 katika miaka ya 1990 hadi chini ya asilimia kumi kwa miaka ya hivi karibuni. Sera ya fedha pia imechangia ukuaji wa uchumi ambao umekuwa ukiongezeka kila mwaka sanjari na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi.

Aidha, Benki Kuu imeshaandaa Kanuni zitakazoongoza uwekaji wa taarifa za watu binafsi pamoja na kampuni (Credit Reference Bureau). Benki Kuu imekwisha tangaza na kukaribisha kampuni zitakazoweka taarifa za wakopaji kuleta maombi ya leseni ya utoaji wa huduma hiyo.

Baadhi ya changamoto ambazo Benki Kuu imekuwa ikikabiliwa nazo ni misukosuko ya uchumi ndani na nje ya nchi, ufinyu wa zana za utekelezaji wa Sera ya Fedha, ufinyu wa masoko ya fedha, ukosefu wa mfumo wa kumbukumbu za wakopaji, ukosefu wa vitambulisho vya uraia na upungufu katika sheria mbalimbali husababisha benki na taasisi za fedha kushindwa kutoa mikopo kwa sekta binafsi kwa kiwango cha kuridhisha.

Pamoja na changamoto hizo, Benki Kuu itaendelea kuboresha utekelezaji wa sera ya fedha, na kuendeleza ushirikiano na Serikali ili kuhakikisha sera ya fedha na sera ya mapato na matumizi ya Serikali zinawiana. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuwa makini na mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika sekta ya fedha duniani na kuweka mfumo madhubuti wa malipo ili kuendeleza utulivu wa sekta ya fedha. Sanjari na hilo, Benki Kuu itaendelea kusimamia utekelezaji wa awamu ya pili ya mageuzi katika sekta ya fedha yanayolenga kuongeza mchango wa sekta ya fedha katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

**Benki ya Rasilimali Tanzania – TIB**

Benki ya Rasimali Tanzania ilianzishwa kwa sheria ya Bunge ya mwaka 1970. Lengo kuu la kuanzisha Benki hii lilikuwa kuwezesha mchakato wa kukuza uchumi kupitia ugharamiaji wa shughuli za maendeleo, hususan katika sekta za viwanda, kilimo na utoaji wa huduma. Kutokana na mtikisiko wa uchumi uliotokea miaka ya 1980 na mageuzi

ya miaka ya 1990 katika sekta ya fedha, Benki ikawa si benki kamili ya kibiashara, iliyopewa leseni chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991.

Serikali ikaifanya Benki kuwa taasisi ya kitaifa ya kugharamia maendeleo mwaka 2005 kwa kutambua mchango muhimu uliotolewa na benki za maendeleo katika maendeleo ya kiuchumi na kwa kutambua pengo linaloongezeka la ukopeshaji wa muda mrefu na wa kati katika uchumi.

Ukuaji wa muda mrefu na endelevu wa uchumi wa Tanzania unategemea pamoja na mambo mengine, upatikanaji wa fedha za kutosha za kugharamia miradi na uwezo wa kutunza na kuhifadhi miradi ambayo huchangia sana katika ukuaji wa haraka wa uchumi.

Majukumu ya Benki ni kuendeleza na kusaidia miradi ya kukuza uchumi; Kupanua wigo wa utoaji wa mikopo; Kuyawezesha mashirika madogo na ya kati kuhimili ushindani katika biashara; na kusaidia kutimiza mahitaji ya kijamii.

**Benki ya Posta Tanzania - TPB**

Benki ya Posta Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 11 ya mwaka 1991 iliyofanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Bunge Na.11 ya mwaka 1992. Benki ilianza shughuli zake rasmi tarehe 1 Machi, 1992 kutoka kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania.

Majukumu ya Benki ya Posta Tanzania ni kukusanya amana na kuhamasisha utamaduni wa kujiwekea akiba miongoni mwa wananchi; Kutoa huduma za kibenki zinazofaa na kukubalika ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kutunza dhamana na nyaraka mbalimbali za kifedha kutoka kwa wananchi; Kusimamia mifuko maalum ya fedha

ambayo imewekwa na wateja au wadau mbalimbali; na kutekeleza majukumu mengine yote ambayo hufanywa na benki za biashara kama vile kutoa mikopo, kusafirisha fedha ndani na nje ya nchi, kuendesha huduma za kibenki kwa njia ya simu za mikononi pamoja na kuuza na kununua fedha za kigeni.

**Twiga Bancorp Limited – TBCL**

Twiga Bancorp Limited ilisajiliwa tarehe 27 Machi 1992 chini ya sheria ya Kampuni na shughuli zake za awali zilikuwa ni biashara ya fedha za kigeni kufuatia kubadilishwa kwa Sheria ya Udhibiti wa fedha za kigeni na kulegezwa baadhi ya masharti ya fedha za kigeni.

Shughuli zinazofanywa na Twiga Bancorp Limited ni kupokea na kutunza amana za wateja kupitia akaunti mbalimbali isipokuwa Akaunti za Hundi; Kutoa mikopo ya aina mbalimbali kwa wateja; Kutuma na kupokea fedha ndani na nje ya nchi kwa niaba ya wateja; na kufanikisha malipo ya biashara kwa niaba ya wateja ndani na nje ya nchi kupitia taratibu za kibenki.

Baadhi ya malengo ya Twiga Bancorp ni Kufungua matawi mengine ili kupanua shughuli za kibiashara. Aidha, baada ya ufunguzi wa Tawi la Mlimani City lililopo Dar es Salaam, Taasisi iko mbioni kufungua matawi mengine Kigamboni - Dar es salaam na Dodoma; na Taasisi itaendelea kubuni huduma mpya kulingana na maendeleo ya teknolojia katika sekta ya fedha na benki ili kuweza kushindana kikamilifu na kuongeza mapato yake.

## Shirika Hodhi la Serikali – CHC

Shirika Hodhi la Serikali lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge ya mwaka 1997 Sura Na. 23.

Majukumu ya Shirika ni kuhodhi, kuwekeza na kusimamia Hisa za Serikali katika NBC Limited kwa niaba ya Msajili wa Hazina; Kupokea na kuendeleza majukumu ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara kuhusiana na mali na madeni ambayo hayakuhamishiwa NBC Limited au NMB Limited; Kupokea na kushughulikia madai na kesi zote za iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara na Mashirika yaliyomaliza muda wake, yaani LART, ATHCO, SIMU 2000 Limited na PSRC; Kufuatilia na kukusanya madeni chechefu yote yaliyopelekwa LART na Wizara ya Fedha au Taasisi za fedha; Ufilisi na Urekebishaji wa Mashirika ya Umma yasiyofanya vizuri; Uuzaji wa mali zilizopokelewa kutoka Mashirika yaliyomaliza muda wake pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa Hati Miliki; Kufanya tathmini na Ufuatiliaji wa mashirika yaliyobinafsishwa na kubinafsisha mashirika ya Umma yaliyoorodheshwa (Specified)

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuuza Mali na Majengo ya iliyokuwa NBC; Kesi zaidi ya 1,496 kati ya kesi 1,928 zimetolewa uamuzi; Uzalishaji bidhaa na huduma umeongezeka kwa kiwango kikubwa katika baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa; Kufuatia kufufuliwa kwa baadhi ya mashirika yaliyokuwa yamefungwa, kumewezesha kutoa fursa za ajira mpya; na mashirika 137 yaliyobinafsishwa yamefanyiwa tathmini. Aidha, tathimini hiyo imesaidia kufanya baadhi ya wawekezaji waliofuatiliwa kuboresha uzalishaji na kuongeza mchango katika pato la Taifa.

Changamoto zinazolikabili Shirika katika utekelezaji wa majukumu yake ni pamoja na baadhi ya wawekezaji kubadili aina ya biashara kinyume na mikataba ya ubinafsishaji

na kuchelewa kukamilisha ulipaji wa madeni kwa mujibu wa mikataba ya mauzo; Madeni kuhusishwa na mashauri Mahakamani, na mengine yakihusishwa na upatikanaji wa hati miliki na hivyo kuchelewesha au kurefusha muda wa ukusanywaji wake; Kuendelea kufunguliwa kwa mashauri mapya na hivyo kusababisha idadi ya kesi kuongezeka; na wawekezaji kutotoa taarifa na kumbukumbu muhimu za utekelezaji wa miradi yao.

## 8.4 Huduma za Bima

### Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – TIRA

Mamlaka ya Usimamizi wa shughuli za Bima ilianzishwa kwa sheria ya Bima Na. 18 ya mwaka 1996. Ilipofika mwaka 2002 sheria hiyo ilibadilishwa na kuwa Sheria ya Bima Sura Na. 394 ya mwaka 2002. Sheria hiyo iliendelea kutumika kwa kipindi cha miaka kumi. Baada ya kubainika kwamba haikidhi kanuni za Kimataifa zinazoongoza soko la bima, Sheria hiyo ilifutwa mwaka 2009 na kutungwa sheria Na. 10 ya mwaka 2009 iliyoanza kutumika Julai 1 mwaka 2009. Sheria hii mpya ndiyo iliyoanzisha Mamlaka ya Bima Nchini.

Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka ni:
Kuweka mazingira mazuri ya ushindani katika soko la bima nchini; Kuiendeleza sekta ya bima na kuifanya kuwa kichochezi cha kukua kwa uchumi wa nchi; Kuweka viwango vya kiutendaji wa kibiashara ndani ya soko la bima; Kuhakikisha soko la bima hapa nchini haliingiliwi; na kuendeleza utendaji mahiri kibima kwa kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo ni za gharama nafuu na zinazomlenga mteja.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kuandaliwa kwa kanuni za kuongoza utatuzi wa madai ya wadau wa bima ili chombo hicho kiweze kuanza kazi ifikapo Julai 1, 2012; Kufanya tafiti mbalimbali zenye lengo la kuishauri Serikali njia bora za kupambana na majanga kwa kutumia huduma ya bima; Kuanzishwa kwa bima ya watu wenye kipato cha chini; Kusimamia soko la bima nchini ili likue na kuchangia uchumi wa taifa kwa kiwango cha asilimia tatu ifikapo mwaka 2014; Kuongeza uwajibikaji katika soko la bima na kuhakikisha madai ya bima yanalipwa inavyotakiwa; Kusogeza huduma za bima vijijini kwa lengo la kuwafikia wananchi wote hii ikiwa ni pamoja na kuuza bima kwa njia ya simu za mkononi na kupitia benki; Soko la Bima kuendelea kuendesha shughuli zake kwa kutumia kanuni za kimataifa ili wawekezaji kutoka nje waweze kukata bima zao hapa nchini, badala ya kukata bima toka nchini mwao; na kutoa elimu ya Bima ili wananchi waliowengi wajue umuhimu wa kukata bima na kujua haki zao.

**Shirika la Bima la Taifa – NIC**

Shirika la Bima la Taifa lilianzishwa tarehe 16 Oktoba, 1963 chini ya Sheria ya Kampuni. Awali, jina la Kampuni lilikuwa Shirika la Bima la Taifa la Tanganyika. Mnamo mwaka 1965 jina hili lilibadilishwa na kuwa Shirika la Bima la Taifa baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mwaka 1967, baada ya kutangazwa kwa **Azimio la Arusha**, Serikali ilichukuwa shughuli zote za Bima. Aidha, tangu kipindi hicho, Shirika la Bima liliendelea kuwa Shirika pekee katika biashara ya bima hadi mwaka 1996 ilipopitishwa sheria ya kuweka huria biashara ya bima nchini Tanzania. Sheria hiyo iliruhusu kampuni binafsi kuleta ushindani katika soko la biashara ya bima.

Kompyuta katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na kwenye ofisi za Mamlaka ili kuboresha utendaji wa soko na mfumo mzima wa usimamizi wa masoko ya mitaji.

Miaka 50
Wizara ya Fedha na Taasisi zake

Mipango ya baadaye ya Mamlaka ni kuzinduliwa kwa Soko la kukuza ujasiriamali kwenye Soko la Hisa Dar es Salaam kwa ajili ya kuorodhesha makampuni ya kati na madogo; Kusaidia uanzishwaji wa Soko la Hatifungani za Manispaa; Kuendeleza Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja na Dhamana za Uwekezaji za Mali isiyohamishika; Kuanzisha Soko la Bidhaa; Kuboresha ushindani kati ya wadau wa masoko; na kushiriki katika hatua za kikanda zenye madhumuni ya ushirikiano katika sheria na muungano wa masoko ya mitaji.

**Dhamana ya Uwekezaji Tanzania – UTT**

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilianzishwa tarehe 19 Juni, 2003, chini ya Sheria ya Bodi ya Wadhamini Sura Na. 318. UTT ilianzishwa kama mrithi wa taasisi ambayo hapo awali ilijulikana kwa jina la Dhamana ya Ubinafsishaji. Dhamana ya Ubinafsishaji ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge iliyotungwa mwaka 1997.

Malengo ya Dhamana hiyo yalikuwa ni kuchukua baadhi ya hisa za Serikali katika mashirika yaliyobinafsishwa kwa ajili ya kuuzwa kwa Umma ili kupata mgawanyiko mpana miongoni mwa wananchi na kupata faida kulingana na hali ya wakati huo; Kuhamasisha na kuunda mazingira ya ushiriki mpana zaidi wa wananchi katika umiliki wa mashirika yaliyokuwa yamebinafsishwa; na kuwajibika katika ulipaji wa faida kulingana na Sheria ya Ubinafsishaji.

## 8.6 Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo

### Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi (FIU)

Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi kiliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu Sura Na. 423, Kifungu cha 4 ya mwaka 2006

Majukumu ya msingi ya kitengo ni kuhakikisha kuwa mfumo wa fedha wa Tanzania hauathiriwi na biashara ya fedha haramu na ufadhili wa Ugaidi kwa kupokea taarifa zenye mashaka juu ya biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kutoka kwa watoa taarifa, kuzifanyia uchambuzi na kisha kuwasilisha matokeo ya uchambuzi kwa vyombo vya kusimamia sheria kwa ajili ya uchunguzi na hatua zaidi za kisheria.

Katika kutekeleza majukumu ya msingi, kitengo kilitekeleza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kutoa miongozo mbalimbali kwa watoa taarifa na kuboresha miongozo iliyopo hususan katika sekta za benki na bima; Kuandaa na kutoa mafunzo juu ya namna ya kupiga vita biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; Kujenga uhusiano mzuri na mawasiliano na wadau wa ndani na nje ya nchi ili kubadilishana taarifa mbalimbali katika vita dhidi ya biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; Kushirikiana na *Australian Transaction Reports and Analysis Centre* (AUSTRAC) katika kutafiti namna bora ya kutoa miongozo ya kudhibiti biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi katika sekta isiyo rasmi; Kuwa na tovuti kwa ajili ya kuufahamisha Umma mambo mbalimbali kuhusu FIU na matukio mengine. Tovuti hii hupatikana kwa anwani ya http//www.fiu.go.tz.

Kitengo kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukaguliwa kwa watoa taarifa kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa; Kushindwa kushiriki moja kwa moja kwenye ukaguzi wa benki mbalimbali kutokana na upungufu wa wafanyakazi; na watoa taarifa wa sekta nyingine hawakaguliwi kutokana na tatizo la uhaba wa wafanyakazi.

Malengo ambayo kitengo kimejiwekea ni pamoja na kushirikiana na wasimamizi na watoa taarifa katika ukaguzi wa sekta ya benki na sekta zingine ili kuhakikisha kuwa sheria zinatekelezwa kikamilifu; Kuhakikisha mfumo wa fedha wa Tanzania hauathiriwi na biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; Kuboresha mfumo wa utawala na rasilimali watu wa kitengo cha FIU; Kuboresha ushirikiano na mawasiliano baina ya kitengo na watoa taarifa, vyombo vya kusimamia utekelezaji wa sheria na wadau wengine ndani na nje ya nchi; na kuboresha usimamizi wa rasilimali na utoaji wa huduma kwa wadau wa kitengo.

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu – NBS**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilianza rasmi mwaka 1999 kama Wakala wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepewa majukumu ya kuendesha, kusimamia na kuratibu shughuli zote za kitakwimu Tanzania Bara. Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kama yalivyoainishwa kwenye kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Takwimu, Na. 1 ya mwaka 2002 ni pamoja na:

Kuendesha Sensa ya Watu na Makazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kuandaa mpango wa kitaifa wa takwimu kwa ajili ya utoaji wa takwimu rasmi za Serikali na

kuuhuisha mara kwa mara; Kuandaa viwango vya kitakwimu na kuhakikisha vinatumika na wazalishaji wote wa takwimu rasmi nchini ili kuleta uwiano na ulinganifu wa takwimu zinazozalishwa ndani ya nchi na kimataifa; Kukusanya na kusambaza takwimu na taarifa zinazohusiana nazo; na kuwa kitovu cha utunzaji na rejea za takwimu zote rasmi nchini kwa Watanzania na Mashirika ya Kimataifa.

Mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni pamoja na kuanzishwa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa kuimarisha na kuboresha Takwimu Tanzania; Kuongeza ubora na kupanua wigo wa uzalishaji wa takwimu za msingi kama vile Pato la Taifa, Mfumuko wa Bei, takwimu za viashiria mbalimbali vya kijamii na kiuchumi; na kuaminika kimataifa katika utoaji takwimu, ambapo Tanzania imechaguliwa kuwa mjumbe kwenye Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2011 hadi 2015.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kada ya watakwimu kwa muda mrefu haikupewa kipaumbele hasa katika upandishwaji vyeo; Mapungufu ya Sheria ya Takwimu Na. 1 ya mwaka 2002 kutotoa uhuru na fursa ya NBS kuelekeza Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kuhusu njia bora za kukusanya takwimu; Ufinyu wa bajeti ya mafunzo na kufungua Ofisi za Takwimu za Wilaya; Ukosefu wa majengo ya uhakika kwa Ofisi za Takwimu mikoani na ufinyu wa ofisi makao makuu; na uhaba wa vitendeakazi.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Ofisi inaazimia kuongeza vitendeakazi; Kufanya ukaguzi mikoani mara kwa mara kuhakikisha takwimu zinazokusanywa zina ubora unaokubalika; Kuandaa mapendekezo ya kuboresha maslahi ya watumishi; na kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

## Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilianzishwa kwa Sheria Na. 33 ya mwaka 1972 na kufanyiwa marekebisho kupitia sheria Na. 2 ya mwaka 1995. Bodi ilianza shughuli zake rasmi mwaka 1973.

Sababu za kuanzishwa kwa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ni uhaba wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kutokana na ukuaji mkubwa wa idadi ya Mashirika ya Umma, Idara za Serikali na asasi mbalimbali za sekta binafsi; Serikali ilikabiliwa na gharama kubwa ya kuelimisha wahasibu nje ya nchi ili kukidhi mahitaji yaliyokuwepo; Wahasibu wageni walioajiriwa kutoka nchi tofauti walikuja na mifumo tofauti ya utayarishaji hesabu iliyoleta tafsiri mbalimbali katika kutoa taarifa za fedha; Hapakuwa na mwongozo mahsusi wa kuelekeza mafunzo ya uhasibu kwenye vyuo vichache vilivyokuwepo. Aidha hapakuwepo chombo chenye mamlaka ya kudhibiti miundo ya mitaala ya mafunzo; Kutokuwa na chombo maalum cha kutoa takwimu kamili za mahitaji ya Wahasibu nchini; na kutokuwepo kwa mamlaka ya kutoa sera, maadili, miiko, na miongozo mbalimbali ya kudhibiti fani ya uhasibu.

Majukumu ya Bodi ni pamoja na kusajili wanachama, kampuni za uhasibu na ukaguzi, na watahiniwa; Kuweka na kudhibiti viwango na miongozo ya uhasibu na ukaguzi; Kuhamasisha na kutoa fursa na nyenzo kwa ajili ya mafunzo ya uhasibu; na kutunga na kusimamia uendeshaji wa mitihani ya uhasibu na ukaguzi.

**Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB**

Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ilianzishwa mwaka 2007 kwa sheria ya Bunge Na. 23. Sheria hii ilifuta sheria Na. 9 ya mwaka 1981 iliyokuwa imeanzisha Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (NBMM). Sheria hizi ziliiipa Bodi jukumu la kusimamia mienendo ya Wataalamu wa fani ya Ununuzi na Ugavi kupitia njia ya usajili, kuratibu mafunzo na kutoa elimu ya fani ya Ununuzi na Ugavi pia kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayohusu taaluma ya Ununuzi na Ugavi.

Mafanikio yaliyopatikana na Bodi ni kuongezeka kwa idadi ya wataalamu pamoja na taasisi zinazotoa mafunzo ya ununuzi na ugavi; Kuandaa mitaala ya mafunzo; Kuanzisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za nje katika fani ya Ununuzi na Ugavi; na kuandaa miongozo mbalimbali ya Ununuzi na Ugavi kwa taasisi za umma sanjari na kutoa miiko na maadili katika utendaji wao wa kazi.

Changamoto zinazoikabili Bodi ni kutotoa wataalamu wa kutosha katika soko la ajira; Kuwepo kwa vikwazo katika utekelezaji wa Sheria mpya Na. 23 ya mwaka 2007 hususani kwa waajiri kuajiri watu wasio na taaluma au fani ya Ununuzi na Ugavi; Sheria haiwabani moja kwa moja waajiri hasa Serikali kuu na Serikali za Mitaa kuhakikisha wanaofanya kazi za ununuzi na ugavi ni waliosajiliwa na Bodi; na Sheria kushindwa kudhibiti mmomonyoko wa maadili miongoni mwa jamii unaoathiri fani ya ununuzi na ugavi.

Matarajio na mwelekeo wa baadaye wa Bodi ni kurekebisha sheria iliyopo ili kuondoa upungufu uliopo kwenye Sheria hiyo.

**Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania – GBT**

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Na. 4 ya mwaka 2003.

Bodi ilianzishwa ili kudhibiti, kuratibu na kusimamia uendeshwaji wa michezo ya kubahatisha nchini. Aidha, majukumu ya Bodi ni kutoa leseni kwa waendeshaji wa aina zote za michezo ya kubahatisha nchini na kuchukua hatua dhidi ya wasiofuata kanuni za leseni hizo; Kuishauri Serikali juu ya kodi na ada zinazotozwa na ukusanyaji wake; Kuandaa sera na maadili ya kitaalamu katika uendeshaji wa michezo; na kuendeleza ushindani wa haki kati ya waendeshaji wa michezo;

changamoto zinazoikabili Bodi ni pamoja na kutokuwa na uwezo wa kuhimili mabadiliko ya teknolojia; na kutopatikana kampuni ya kuendesha Bahati Nasibu ya Taifa kwa mafanikio.

**Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA**

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura Na. 399 kifungu cha 4. Sheria hiyo ilianza kutumika mnamo mwaka 1995 kwa tangazo la Gazeti la Serikali Na. 419 la mwaka 1995.

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilirithi shughuli zilizokuwa zinatekelezwa na Idara za Kodi chini ya Wizara ya Fedha kuanzia mwaka 1996. Jukumu kuu la Mamlaka ya Mapato ni kukusanya mapato ya Serikali.

Kufuatia kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, makusanyo ya kodi yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka.

Changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Mapato Tanzania ni pamoja na kuhakikisha malengo ya makusanyo ya kodi yanafikiwa; Watu wote wanaostahili kulipa kodi wanalipa kodi stahili na kwa muda muafaka; na ukwepaji na uvujaji wa malipo ya kodi.

Malengo ya baadaye ya Mamlaka ni kutoa elimu ya kodi kwa umma ili walipakodi watimize wajibu wao; Kupanua wigo wa kodi katika sekta binafsi na kuongeza makusanyo ya kodi kwa ujumla; na kuhakikisha mianya ya ukwepaji kodi inazibwa.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma – PPRA**

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imeanzishwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004. Kutungwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ilikuwa ni sehemu ya uboreshaji uliopendekezwa mwaka 2002 wakati wa mapitio ya utaratibu mzima wa ununuzi wa Umma.

Malengo ya kuboresha mfumo wa sheria na udhibiti yalikuwa ni kuondokana na mfumo wa ununuzi wa pamoja chini ya iliyokuwa Halmashauri Kuu ya Tenda na kuzipa taasisi za Umma uwezo wa kufanya ununuzi wao wenyewe ili kuongeza uwazi na uwajibikaji; Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kama chombo cha kudhibiti na kusimamia sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa Umma; Kuweka mfumo wa kushughulikia malalamiko ya wazabuni na kuanzisha Mamlaka ya Rufaa za Zabuni; na kuondoa ukomo wa viwango vya ununuzi.

## Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma – PPAA

Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma ilianzishwa chini ya iliyokuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Na. 3 ya Mwaka 2001 na kuanza kazi rasmi mwezi Novemba, 2004 na muda mfupi baadaye Sheria hiyo ilifutwa kwa Sheria Na. 21 Sura Na. 410 ya mwaka 2004.

Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni kutoa nafasi kwa wazabuni kuwa na chombo cha kutatua na kusikiliza malalamiko yao juu ya michakato ya ununuzi wa Serikali na Taasisi zake nje ya utaratibu wa mahakama kama njia ya kuharakisha utatuzi wa migogoro ili kutoathiri utekelezaji wa miradi ya Serikali.

Majukumu ya Mamlaka ni kupokea rufaa na malalamiko kutoka kwa wazabuni dhidi ya uamuzi wa taasisi za ununuzi au uamuzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma; Kufanya mapitio juu ya mchakato wa ununuzi unaolalamikiwa kwa kusikiliza pande husika na kufanya uchambuzi wa nyaraka na taratibu zilizotumika kwa lengo la kutatua mgogoro na kuhakikisha kuwa ufumbuzi unapatikana kwa haraka bila kuathiri utekelezaji wa mradi husika; na kuagiza marekebisho yafanyike pale inapoonekana kuwa taasisi ya ununuzi ilikiuka sheria katika uamuzi wake na kutoa ufafanuzi juu ya maeneo yasiyoeleweka baina ya pande zinazolumbana.

Tangu kuanzishwa kwake Mamlaka imefanikiwa kupokea na kushughulikia malalamiko 112 yaliyotokana na zabuni za Serikali na Taasisi.

Mipango ya baadaye ya Mamlaka ni kuongeza juhudi za uelimishaji kwa wafanyabiashara wanaotoa huduma mbalimbali Serikalini ili kuwapa uelewa wa haki zao pindi wanaposhiriki katika ununuzi serikalini.

## Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – GPSA

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kutangazwa katika gazeti la Serikali Na. 235 la tarehe 7 Disemba, 2007 na kuzinduliwa rasmi mwaka 2008.

Mafanikio yaliyopatikana na Wakala tangu kuanzishwa kwake ni pamoja na kuwa na Ofisi katika mikoa yote ya Tanzania Bara; Ongezeko la wataalamu wenye elimu ya juu katika kada ya ugavi nchini; na gharama za ununuzi Serikalini zimepungua kwa kuwa Wizara, Idara na Taasisi zinatangaza zabuni zake kupitia GPSA.

Changamoto zinazoukabili Wakala ni pamoja na upungufu wa fedha; Kutokuwa na uelewa wa kutosha kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu shughuli zinazofanywa na Wakala; na kuchakaa kwa majengo yanayotumiwa na Wakala.

Matarajio ya baadaye ya Wakala ni kuongeza rasilimali watu na vitendeakazi; kukusanya na kutangaza maombi ya zabuni kwa njia ya mtandao; na kuongeza wigo wa kutoa huduma hadi kufikia ngazi ya Wilaya.

## Mpango wa Millennium Challenge Account Tanzania-MCA(T)

Mpango huu ulianzishwa kwa tangazo la Serikali Na. 202 la tarehe 21 Septemba 2007 kama chombo chenye mamlaka ya kisheria ya kusimamia utekelezaji wa miradi na shughuli za MCA-T zinazopata fedha kutoka Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Millennium Challenge Corporation-(MCC)

Lengo la miradi ni kuchochea ukuaji wa uchumi, kuinua kipato na kuleta maisha bora kwa wananchi katika ujumla wao kwa kuimarisha miundombinu katika sekta za usafirishaji, nishati na maji ambayo inatekelezwa kwenye mikoa 15, ikiwemo mikoa 11 ya Tanzania Bara na mikoa 4 ya Tanzania Visiwani.

Baada ya kukamilika uboreshaji wa miundombinu katika sekta za usafirishaji, nishati na maji matarajio ni kupungua kwa gharama za usafirishaji na muda wa kusafiri; Ongezeko la wasafiri wa ndege; Ongezeko la nishati ya umeme wa kuaminika; Ongezeko la idadi ya kaya na biashara zitakazotumia maji salama

**Tume ya Pamoja ya Fedha – JFC**

Tume ya Pamoja ya Fedha imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Mwaka 1996 Sura Na.140. Tume ilianza kutekeleza kazi mwaka 2003.

Majukumu ya Tume ni kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 133 na 134 ya Katiba. Majukumu hayo ni kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo; Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili; na kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza, na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kutoa mapendekezo kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano; Kufanya utafiti kwa

lengo la kutoa ushauri wa kitaalam na mapendekezo kwa Serikali mbili.

Katika kutekeleza majukumu yake Tume imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni kutokuwepo utaratibu mahsusi wa jinsi Serikali mbili zitakavyoshughulikia ushauri na mapendekezo ya tume; Kukosekana utaratibu wa kubainisha gharama za utekelezaji wa Mambo ya Muungano; Kutofunguliwa kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa mujibu wa Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Sheria ya Tume iliyotungwa mwaka 1996 na kuanza kutumika mwaka 2003 inahitaji kufanyiwa mapitio.

**Bodi ya Rufaa za Kodi – TRAB**

Bodi ya Rufaa za Kodi imeundwa kwa sheria ya Rufaa za Kodi ya mwaka 2000 kwa lengo la kushughulikia migogoro yote ya kodi baina ya mlipakodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mafanikio ya Bodi tangu kuanzishwa kwake ni pamoja na kutatua migogoro ya kodi mapema zaidi ukilinganisha na hapo awali kabla ya kuundwa kwake; Kupitia uamuzi wa Bodi, wadau wake wanapata elimu ya sheria husika hivyo kujua taratibu za kukata na kusikiliza rufaa za kodi katika Bodi; na kutoa ripoti za mwenendo na uamuzi wa rufaa za kuanzia Mwaka 2002 hadi 2004 ambazo zinasaidia kutoa ufafanuzi wa sheria mbalimbali za kodi kwa wadau.

Bodi imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni ufinyu wa Bajeti inayotengwa kwa shughuli za Bodi na hivyo Bodi imejikuta ikishindwa kufikia malengo iliyojiwekea katika utekelezaji wa majukumu yake; Ufinyu wa vyumba vya ofisi, kumbi za kusikilizia kesi na vyumba vya kupumzikia wateja wanaposubiri kuingia kwenye vyumba

vya mashauri; na huduma za Bodi zinapatikana mbali na wateja kwani wahusika hulazimika kufikisha rufaa zao Ofisi kuu ya Dar es Salaam.

Bodi ina mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Mikakati hiyo ni pamoja na kupata ufumbuzi wa kudumu juu ya tatizo la vyumba vya Ofisi; na kufungua Ofisi za kanda ili kufikisha huduma karibu zaidi na wadau.

Matarajio ya baadaye ya Bodi ni kuendelea na utatuzi wa migogoro ya kodi; Kuendelea na zoezi la kutoa elimu kwa wadau; na kupata kiwanja kwa ujenzi utakaokidhi mahitaji ya Ofisi.

**Baraza la Rufaa za Kodi – TRAT**

Baraza limeanzishwa kwa sheria ya Rufaa za Kodi ya mwaka 2000 kwa lengo la kushughulikia migogoro yote ya kodi inayotokana na uamuzi ya Bodi ya Rufaa za Kodi kwa haraka.

Majukumu ya Baraza ni pamoja na kupokea, kusikiliza na kutolea uamuzi wa migogoro ya kodi itokanayo na uamuzi wa Bodi ya Rufaa za Kodi; Kutoa ushauri kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipa kodi juu ya taratibu za kukata na kusikiliza rufaa za kodi; na kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria ya Rufaa za Kodi na kanuni zake.

Mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Baraza ni pamoja na kutoa uamuzi mapema iwezekanavyo kwa wastani wa asilimia 90 ya rufaa zinazopokelewa kila mwaka; Kupitia uamuzi wa Baraza, walipa kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania na umma kwa ujumla wanapata elimu ya sheria mbalimbali za kodi hivyo kurahisisha ulipaji na ukusanyaji wa kodi; Kutoa vitabu vya Taarifa za Kodi ambavyo vinasaidia kutoa ufafanuzi wa sheria mbalimbali

za kodi kwa wadau; na kutoa elimu kwa wadau katika makao makuu ya mikoa yote Tanzania Bara na baadhi ya wilaya juu ya utaratibu mzima wa kukata rufaa za kodi.

Baraza lina matarajio ya kufungua ofisi za kanda ili kufikisha huduma kwa jamii; Kuendelea na utatuzi wa migogoro ya kodi kwa kadri inavyolifikia; Kuendelea na zoezi la kutoa elimu kwa wadau kwa lengo la kufikisha elimu hiyo katika wilaya zote Tanzania Bara; na kupata kiwanja kwa ajili ya ujenzi utakaokidhi mahitaji ya ofisi.

## 8.7 Asasi za Mafunzo

### Taasisi ya Uhasibu Arusha – IAA

Taasisi ya Uhasibu Arusha ilianzishwa rasmi kwa sheria ya Bunge Na. 1 ya mwaka 1990.

Majukumu ya Taasisi ya Uhasibu Arusha ni pamoja na kutoa mafunzo katika ngazi za cheti, stashahada, stashahada za Juu, Shahada na Shahada za Uzamili katika fani za Uhasibu, Kodi, Sayansi ya Kompyuta, Teknolojia ya Habari, Usimamizi wa fedha na Ugavi na Rasilimali; na kufanya utafiti na Kutoa ushauri.

Mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa taasisi ni pamoja na kutoa mafunzo katika shahada saba ambazo ni Shahada ya Uhasibu, Shahada ya Usimamizi wa Fedha na Benki, Shahada ya Usimamizi wa Uchumi na Fedha, Shahada ya Ugavi na Usimamizi wa Rasilimali, Shahada ya Usimamizi wa Biashara, Shahada ya Teknolojia ya Habari na Shahada ya Sayansi ya Kompyuta; Kuanzisha stashahada sita katika kada za Uhasibu, Usimamizi wa Fedha na Benki, Ugavi na Usimamizi wa Rasilimali, Usimamizi wa Biashara, Teknolojia ya Habari na Sayansi ya Kompyuta.

Aidha katika ngazi ya Cheti Taasisi imeongeza kozi nyingine tatu ambazo ni Usimamizi wa Fedha na Benki, Ugavi na Usimamizi wa Rasilimali na Usimamizi wa Biashara; Taasisi imeanzisha shahada mbili za uzamili, moja ya Ugavi na Upangiliaji Rasilimali (MBA LM) na nyingine ni ya Habari na Mawasiliano (MBA ITM) kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Coventry cha Uingereza; Taasisi imeanzisha kampasi Dar es Salaam na tayari imeanza kutoa mafunzo katika ngazi ya shahada ya uzamili; na kubadilisha uendeshaji wa mafunzo kutoka mafunzo ya nadharia kwenda mafunzo ya vitendo *"competence based"* katika ngazi ya cheti hadi shahada.

Taasisi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni ongezeko kubwa la wanafunzi linalosababisha kuwepo na uhitaji wa kujengwa kwa madarasa mengine haraka iwezekanavyo; Uhitaji mkubwa wa wahadhiri wengi na wenye sifa ili kuweza kukidhi viwango vinavyohitajika; Fedha nyingi zinahitajika katika kuwaendeleza wahadhiri hasa katika ngazi ya udaktari; na Upungufu wa mabweni.

Matarajio ya taasisi ni kuendelea kutoa taaluma bora na yenye tija; Kutoa shahada za udaktari katika kozi za Uhasibu, Uchumi, Biashara, Teknolojia ya habari na kompyuta; Kuanzisha kampasi katika mikoa yote mikubwa nchini kwa ajili ya kutoa mafunzo; Kujenga tawi la Chuo Babati kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa ngazi ya cheti na stashahada; na kuwa kitovu cha taaluma bora ya masuala ya Uchumi na Teknolojia ya Habari, kusini mwa Jangwa la Sahara.

## Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA

Taasisi ya Uhasibu Tanzania ilianzishwa Julai 2002 kupitia Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997, ikiwa ni sehemu ya mabadiliko ya utendaji wa taasisi za Umma chini ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma.

TIA ilianzishwa kuchukua nafasi ya kilichokuwa Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam (DSA) ambacho kilianzishwa rasmi tarehe 01 Januari mwaka 1973 kama Idara katika Wizara ya Fedha, chini ya Agizo Maalum la Wizara. DSA ilikuwa na majukumu ya kuendesha Kozi fupi na ndefu kwenye nyanja za Uhasibu na Ugavi kwa wafanyakazi wa ngazi ya chini na kati ili kuboresha utendaji mahali pa kazi.

Chuo kina majukumu muhimu ya kutoa mafunzo katika nyanja za Uhasibu, Ununuzi , Ugavi na maeneo mengine ya kibiashara; Kutoa na kufanya tafiti na ushauri katika nyanja za Uhasibu, Ununuzi, Ugavi na maeneo mengine ya kibiashara; Kuzalisha mapato ili kukidhi angalau asilimia hamsini (50%) ya bajeti yake kwa lengo la kujitegemea.

Mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Chuo hadi sasa ni pamoja na kupanua wigo wa elimu kutoka kozi mbili (2) mwaka 1995 hadi 14 kwa mwaka 2011; Kuongeza majengo ili kutoa huduma kwa ufanisi; Kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 500 hadi 5000 kwa mwaka 2011; Kuboresha Mitaala ili kuendana na wakati uliopo; na kuwaendeleza wafanyakazi wake kitaaluma.

**Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM**

Chuo kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 3 ya mwaka 1972, kwa lengo la kutoa mafunzo katika fani za Benki na Bima. Kuanzishwa kwa chuo hiki kulitokana na umuhimu wa kuwaandaa wataalamu katika fani za Benki na Bima kufuatia utaifishaji wa sekta za Benki na Bima.

Chuo kilianza shughuli zake rasmi mwezi Julai mwaka 1972 kikiwa na idadi ya wanafunzi 72 walioandikishwa kwenye kozi za Benki na Bima. Kufuatia mahitaji ya wataalamu

katika fani za fedha, idadi ya kozi iliongezeka kutoka mbili wakati Chuo kilipoanzishwa hadi kufikia kozi 22 mwaka 2010.

Majukumu ya chuo ni pamoja na kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri kwa jamiii katika fani za Benki, Bima, Udhibiti Majanga, Kodi na Uhasibu; Kutoa mafunzo yanayolenga kutoa tuzo za kitaalamu katika fani za Benki, Bima, Usimamizi wa Fedha; Kudhamini, kuandaa na kutoa huduma kwa ajili ya mikutano na semina; na kuandaa taratibu kwa ajili ya machapisho na usambazaji wa majarida mbalimbali yanayohusiana na kazi na shughuli za Chuo.

**Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – IRDP**

Chuo kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 8 ya mwaka 1980, kama kituo cha Taifa cha kutoa mafunzo , kufanya utafiti, na kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika mipango ya maendeleo vijijini. Chuo kilianza rasmi mnamo mwaka 1979, kwa lengo la kuongeza utaalamu wa upangaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo karibu na wananchi vijijini.

Majukumu ya Chuo ni pamoja na kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika nyanja zote za mipango ya maendeleo hasa vijijini; Kufanya utafiti katika mada mbalimbali zinazolenga katika kuleta maendeleo kwa jamii; Kukusanya takwimu na taarifa zote muhimu za mipango ya maendeleo hasa vijijini; na kutoa ushauri na uelekezi katika mipango ya maendeleo.

Mafanikio yaliyopatikana hadi sasa ni pamoja na kuongeza idadi ya programu za mafunzo ya muda mrefu kutoka programu 2 hadi 10; Kuongezeka kwa idadi ya wanachuo wanaojiunga na kuhitimu mafunzo mbalimbali. Chuo

kilipoanzishwa Mwaka 1979 kilikuwa na wanafunzi 22, ambapo kwa sasa chuo kina wanafunzi 4264; Kukuza uwezo wa rasilimali watu kwa kuendeleza wafanyakazi kitaaluma na kitaalamu; Kuongeza ushirikiano na Wabia wa Maendeleo; na kuanzisha kituo cha mafunzo cha Kanda ya Ziwa Mwanza.

Chuo kinakabiliwa na changamoto mbalimbali, miongoni mwa changamoto hizo ni ongezeko kubwa la wahitaji wa mafunzo yanayotolewa ambalo haliendi sanjari na miundombinu iliyopo; na mahitaji ya rasilimali watu ili kuendana na ongezeko la wanafunzi.

Malengo ya baadaye ya Chuo ni kuendelea kuwa kituo madhubuti cha kutoa mafunzo, utafiti, ushauri na uelekezi katika mipango ya maendeleo ndani na nje ya nchi; Kuwa na uwezo wa kutoa mafunzo katika nyanja zote za mipango ya maendeleo ili kukidhi mahitaji ya wadau wa maendeleo; Kuanzisha vituo zaidi vya kanda vya mafunzo na habari; Kutoa mafunzo hadi kufikia kiwango cha shahada za uzamivu; na kuongeza kasi ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ili kuwezesha utoaji wa huduma na majukumu ya Chuo kwa ufanisi.

**Chuo Cha Takwimu Mashariki mwa Afrika - EASTC**

Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kilianzishwa mwaka 1965 na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNPD) kwa kushirikiana na shirikisho la nchi za Afrika Mashariki. Madhumuni ya Chuo ni kufundisha Takwimu kwa wafanyakazi wa Ofisi za Takwimu za nchi wanachama, yaani Kenya, Tanzania na Uganda. Baada ya kuvunjika jumuiya ya Afrika Mashariki 1977 chuo kiliwekwa chini ya Serikali ya Tanzania, ambayo ilitunga sheria Na. 28 ya mwaka 1994, na baadaye kuwa wakala wa Serikali chini ya sheria Na. 30 ya mwaka 1997.

Majukumu ya chuo yanalenga kwenye kuhamasisha matumizi ya takwimu katika mipango na kuhimiza uzalishaji na usahihi wa taarifa za kitakwimu; Kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za tafiti zenye ubora wa hali ya juu; Kushiriki na kutoa ushauri wa kitakwimu; na kuendeleza Chuo kuwa wakala wenye ubora na umakini katika kutoa huduma.

Mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa Chuo ni pamoja na uboreshaji wa mafunzo kwa kutumia mafunzo kwa vitendo; Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa ndani na nje ya nchi; Marejeo ya mitaala ya Cheti na Stashahada ili ifundishwe kwa utaratibu wa moduli; na kutoa ushauri wa mifumo ya takwimu kwa Wizara, Idara na taasisi za serikali.

Chuo kinakabiliwa na changamoto mbalimbali, miongoni mwa changamoto hizo ni Kupungua kwa wanafunzi wanaofadhiliwa na Serikali za nchi zinazotumia huduma ya chuo, hivyo kufanya usajili wa wanafunzi kushuka; Kutokuwepo na mfumo wa kusimamia watakwimu katika Wizara na Idara zinazojitegemea; Wafanyakazi wataalamu kubadili fani ya Takwimu, na kuingia kwenye fani nyingine; Jamii haijahamasika kuhusu matumizi ya Takwimu, hivyo kuipa takwimu nafasi ndogo kwenye maisha; Kupungua idadi ya wahitimu wa kidato cha nne (kwa Tanzania) wanaofaulu somo la Hisabati na Kiingereza, hivyo kukosa sifa za kusajiliwa chuoni; Uwepo wa tofauti ya mitaala inayotumiwa na nchi zinazotumia huduma ya Chuo na kianzio kimoja cha fedha za kutekeleza Mpango Mkakati wa Upanuzi (Master Plan 2020) wa chuo.

Matarajio ya baadaye ya Chuo ni Kukikuza chuo na kupanua huduma za chuo ili kiweze kuhudumia nchi zote za Afrika; Kuwapunguzia wadau gharama za mafunzo kwa

kuanza mafunzo ya mtandao (E-Learning); Kuongeza idadi ya kozi za takwimu na kuanzisha kituo cha utafiti kwa nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika.

## 9.0 SERA NA SHERIA ZILIZOKUWEPO TANGU UHURU HADI SASA

### 9.1 SERA

Wizara imekuwa ikitekeleza sera mbalimbali tangu wakati wa kupata Uhuru mwaka 1961. Sera zilizotungwa na kutekelezwa na Wizara tangu wakati kuo ni pamoja na:

**Sera za Kodi na Mapato.**

Baada ya kupata Uhuru, Serikali ilianza kutekeleza sera za kodi na mapato kwa lengo la kukusanya mapato ya kutosha. Wananchi walihamasishwa kulipa kodi na pia Serikali ilifuta kodi zilizokuwa zinawadhalilisha. Kodi zilizofutwa ni kodi ya kichwa (hat and polls taxes), tozo na leseni ambazo ukusanyaji wake ulikuwa unadhalilisha wananchi.

Aidha, Serikali iliendelea kuboresha sheria za kodi na kuimarisha usimamizi wake kwa nia ya kuongeza makusanyo ya kodi kwa kuzingatia uwezo na kipato cha walipa kodi.

Sera za kodi zimeendelea kuwa nyenzo muhimu ya kuchochea ukuaji wa uchumi ambapo unafuu wa kodi hutolewa kwa sekta mbalimbali za uchumi hususan kilimo, viwanda, biashara, madini, na usafirishaji.

Hatua mbalimbali zimechukuliwa kuimarisha usimamizi wa kodi na kuufanya mfumo wake kuwa na ufanisi zaidi na wa kisasa, zikiwemo kurekebisha mara kwa mara sheria za kodi, kutunga sheria mpya za kodi, kupunguza viwango vya kodi na kufuta baadhi ya kodi ambazo zimeonekana kuwa kero kwa wananchi.

Katika jitihada za kuimarisha ukusanyaji mapato, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mnamo mwaka 1996 kwa Sheria ya Bunge ya mwaka 1995 Sura ya 399 ikiwa ni chombo cha kusimamia na kuratibu ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi za Serikali Kuu.

Sheria na viwango vya ushuru wa forodha vimerekebishwa ili kulinda viwanda vya ndani, kurahisisha biashara za kimataifa, na kuchochea kukua kwa uchumi. Hatua hizi zilienda sanjari na kutekeleza sera za kuimarisha biashara ya kikanda na kimataifa, ambapo Serikali ilianzisha majadiliano ya kuwianisha ushuru wa forodha baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Majadiliano haya yamewezesha kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Custom Union) na Ukanda wa Biashara Huru wa nchi za Kusini mwa Afrika (SADC Free Trade Area).

Pamoja na uboreshaji wa sera za kodi, mabadiliko makubwa yalifanywa kuanzia kipindi cha mwaka 1995/96 ambapo sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipitishwa na mamlaka hiyo kuanzishwa mwaka 1996. Kufuatia kuanzishwa kwa mamlaka hiyo, kumekuwepo na ongezeko kubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ambapo katika kipindi cha mwaka 1995/96 mapato ya ndani yalikuwa shilingi milioni 446,750.2 ambapo yaliongezeka kufika kiasi cha shilingi milioni 929,624.0 katika kipindi cha mwaka 2000/01 na kufikia shilingi milioni 4,654,872.5 katika mwaka 2010/11.

## SERA ZA FEDHA NA VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

### Kipindi Kabla ya Uhuru

Kabla ya uhuru, Tanganyika haikuwa na Benki Kuu. Katika kipindi hiki, jukumu la kusimamia ujazi wa fedha Tanganyika linaweza kugawanywa katika vipindi viwili tofauti: kipindi cha mwanzo wa karne ya ishirini ambacho jukumu hilo lilikuwa chini ya kampuni ya kikoloni ya Kijerumani itwayo Deutsch-Ostafrikanische Gesellschaft hadi mwaka 1903 ambapo jukumu hilo lilichukuliwa na serikali ya Kijerumani. Sarafu iliyokuwa inatumika wakati huo iliitwa Rupia.

Kipindi cha pili ni baada ya vita kuu ya kwanza ya dunia (1914-18) ambapo Tanganyika iliwekwa chini ya udhamini wa serikali ya Uingereza. Jukumu hilo liliwekwa chini ya Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki (The East African Currency Board) iliyoanzishwa mwaka 1919. Sarafu ya Rupia iliondolewa na kuanzishwa mfumo wa Paundi/shilingi mwaka 1921.

Kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi, hasa kuanzia miaka ya 1950, kulisababisha ongezeko la mabenki nchini ili kukidhi mahitaji ya huduma za kifedha. Sanjari na ongezeko hilo, majukumu ya Bodi ya Sarafu yaliongezeka kutoka katika usimamizi wa ujazi wa fedha hadi utoaji wa mikopo kwa benki ili kuwezesha uzalishaji wa bidhaa za kilimo zilizokuwa zinauzwa nje ya nchi.

### Kipindi Baada ya Uhuru

Baada ya Uhuru wa Tanganyika Desemba 1961, matukio ya utoroshwaji wa mitaji na amana katika benki yaliendelea hivyo, mahitaji ya mikopo yalizidi uwezo wa benki

kukopesha. Hali hii ilipelekea kuvunjwa kwa Bodi ya Sarafu 1966 na kuanzishwa kwa Benki Kuu katika nchi za Kenya, Tanzania na Uganda.

Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa kwa sheria ya mwaka 1965 na kupewa uwezo wa kutekeleza majukumu yote ya msingi. Hata hivyo, muda mfupi baada ya kuanzishwa kwa Benki Kuu, Azimio la Arusha likatangazwa mwaka 1967 na kuweka njia zote za uchumi chini ya umiliki wa sekta ya umma. Hali hii ilibadilisha mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu na shughuli za Benki Kuu ya Tanzania.

Katika kipindi hicho, sera ya fedha ilitegemea maelekezo kutoka Serikali Kuu kupitia miongozo ya fedha na mikopo na ile ya fedha za kigeni iliyoanzishwa mwaka wa fedha 1971/72. Miongozo hii iliandaliwa kwa pamoja na iliyokuwa Wizara ya Mipango ya maendeleo na Benki Kuu. Benki Kuu iliwajibika kutekeleza miongozo hiyo kwa mujibu wa sheria za fedha za kigeni na ile ya udhibiti wa uagizaji wa bidhaa nje iliyorekebishwa na sheria ya fedha ya mwaka 1973.

Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1965 ilifanyiwa marekebisho mnamo mwaka 1978, ili kuipa Benki Kuu uwezo wa kukabiliana na mabadiliko na changamoto zilizojitokeza katika kusimamia mabadiliko ya uchumi. Chini ya marekebisho hayo, Benki Kuu ilianzisha mifuko minne maalumu iliyojulikana kama: Rural Finance Fund, Industrial Finance Fund, Export Credit Guarantee Fund, na Capital and Interest Subsidy Fund. Mifuko hiyo ilianzishwa ili kuwezesha upatikanaji wa fedha na dhamana kwa benki na taasisi nyingine za kifedha dhidi ya mikopo iliyotolewa kwenye sekta mbalimbali za uchumi. Aidha, mabadiliko hayo yaliipa uwezo Benki Kuu kukagua na kusimamia shughuli za benki na taasisi za fedha nchini.

Kwa ujumla wake, miaka ya 1960 na 1970 ilihusishwa na udhibiti wa moja kwa moja wa sera ya fedha, udhibiti wa mikopo, riba na fedha za kigeni. Aidha, kulikuwa na ongezeko la mikopo ya serikali iliyozidi kiwango, ongezeko la mikopo chechefu katika mabenki ya biashara na usimamizi hafifu wa shughuli za mabenki na taasisi za fedha nchini. Hali hii ilisababisha kudhoofu kwa mfumo wa fedha uliohusishwa na: kasi kubwa ya mfumuko wa bei, ongezeko la riba, kushuka kwa mapato ya rasilimali za benki, kuongezeka kwa ulanguzi katika masoko ya fedha na matumizi ya fedha taslimu kwenye uchumi. Upungufu huo ulisababisha kuwepo kwa haja ya kufanya mageuzi makubwa katika uchumi, hususan katika sekta ya fedha, kuanzia miaka ya 1980.

**UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA KWA MISINGI YA SOKO**

Mabadiliko yalianza kujitokeza baada ya kupitishwa na Bunge sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995. Chini ya sheria hii Benki Kuu ilipewa mamlaka ya kutekeleza sera ya fedha inayozingatia misingi ya soko huria. Sera hii ndiyo inayotumika hadi sasa.

Katika kutekeleza malengo ya sera ya fedha, Benki Kuu inatumia mchanganyiko wa zana za sera zikiwemo: mauzo ya dhamana na hati fungani za serikali, mauzo ya fedha za kigeni, mikataba ya kununua upya na madirisha yake ya ukwasi.

Benki Kuu inatumia mfumo wa kulenga ujazi wa fedha, unaolenga kuendeleza utulivu wa bei na kudumisha kiwango sahihi cha ukwasi katika uchumi. Mfumo huu unatumika sanjari na hali halisi ya ukuaji wa masoko ya fedha, na upatikanaji wa takwimu za kiuchumi. Benki Kuu huweka malengo yake ya mwaka ya ujazi wa fedha

ambayo huchapishwa kama tamko la sera ya fedha na kuwasilishwa kwa waziri wa fedha, na hatimae kuwasilishwa bungeni. Malengo hayo ambayo hulenga kufikia malengo ya kitaifa ya ukuaji wa Pato la Taifa na lengo la mfumuko wa bei, hufanyiwa mapitio kila baada ya miezi sita kuhakikisha kwamba yako sanjari na malengo yaliyo kusudiwa.

## MAFANIKIO YA SERA YA FEDHA

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa sera ya fedha hasa katika kipindi cha mwaka1995 hadi 2010 ni pamoja na kukua kwa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 2.3 mwaka 1978 hadi 1994; Kushuka kwa mfumuko wa bei hadi kufikia asilimia 10.0 kutoka wastani wa asilimia 27.6 katika mwaka 1978 hadi 1994; Uwepo wa ukuaji wa wastani wa ujazi wa fedha wa asilimia 19.5 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 28.7 katika miaka ya 1978 hadi 1994; na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi sanjari na ukuaji wa uchumi.

## MABADILIKO KATIKA SERA YA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

Tanzania ilichagua kuwa na kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni ambacho hakibadiliki (fixed exchange rate) kilichokuwa kimefunganishwa na Paundi ya Uingereza. Chini ya mfumo huo Shilingi ya Tanzania ilifunganishwa na Paundi katika kiwango cha Shilingi za Kitanzania 20 sawa na Paundi 1. Kiwango hiki kiliendelea kutumika chini ya usimamizi mkali wa ubadilishanaji wa fedha za kigeni. Kufuatia kupunguzwa kwa thamani ya Paundi hapo Novemba 1967, Serikali iliamua kuifunganisha shilingi ya Tanzania kwenye sarafu nyingine yenye nguvu zaidi ambayo kwa wakati huo ilikuwa Dola ya Marekani ambapo ilifunganishwa katika kiwango cha shilingi za Kitanzania 7.14286 sawa na Dola 1 ya Kimarekani.

Ilipofika Oktoba 1975 Serikali ilihamisha kuifunganisha shililingi ya Tanzania kutoka Dola ya Marekani kwenda Special Drawing Rights (SDR) na hii ilitokana na kushuka kwa thamani ya dola kwa wakati huo. Kufunganishwa kwa Shilingi ya Tanzania na SDR kuliendelea hadi ilipofika mwaka 1979, ambapo shilingi ya Tanzania ilifunganishwa na kapu la sarafu ambazo kwa wakati huo zilikuwa ni sarafu za nchi tulizofanya nazo biashara kwa wingi, na sababu ya kufanya hivyo ilikuwa kwamba SDR ziliongezeka thamani ikilinganishwa na Dola ya Marekani hivyo kwa kiasi fulani ilipunguza ushindani wa bidhaa zetu tunazouza nje ya nchi.

Mwanzoni mwa mwaka 1982 kwa kiasi kikubwa shilingi ya Tanzania ilipunguzwa thamani ili kupunguza kiwango ambacho hakikuwa halisi cha ubadilishanaji fedha za kigeni na kupunguza nakisi iliyokuwepo kwenye Urari wa Malipo (Balance of payment) katika uchumi wetu. Thamani ya Shilingi ilishuka kutoka Shilingi 12.5 kwa Dola 1 mwaka 1982 hadi Shilingi 196.6 kwa Dola 1 mwaka 1990.

Miaka ya 1990 ilikuwa ndiyo miaka ya mabadiliko makubwa katika historia ya sera ya viwango vya ubadilishanaji fedha za kigeni baada ya kugundua kuwa kuweka viwango vya kubadilisha fedha za kigeni hakuwezi kuhimili misukosuko ya kiuchumi iliyokuwa imeikabili nchi yetu katika kipindi hicho. Sheria ya kubadilisha fedha za kigeni ya mwaka 1991 (Foreign Exchange Act 1991) ilianzishwa ili kuchukua nafasi ya Sheria iliyokuwepo ya Udhibiti wa Fedha za Kigeni ya mwaka 1965 (Exchange Control Ordinance of 1965) ambayo ilikuwa haiendani na mabadiliko ya kiuchumi yaliyokuwa yamefanywa kuanzia miaka ya 1980. Sheria hii iliruhusu kuanzishwa kwa maduka binafsi ya kubadilisha fedha ilipofika Aprili 1992, kuanzishwa kwa minada ya fedha za kigeni Julai 1993 na kuanzishwa kwa Soko la Mabenki la

Fedha za Kigeni (Interbank Foreign Exchange Market - IFEM) Juni 1994.

Mfumo huu wa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni umejengwa kwenye kanuni za soko huria la fedha za kigeni ambao unategemea maendeleo katika Soko la Mabenki la Fedha za Kigeni (Interbank Foreign Exchange Market - IFEM). Kiwango rasmi cha kubadisha fedha za kigeni kinategemea hali ya kibiashara katika Soko hilo. Kufuatia kuanzishwa kwa soko huria la fedha za kigeni, watu binafsi waliruhusiwa kuwa na fedha za kigeni na kufungua akaunti za fedha za kigeni katika benki za biashara nchini Tanzania.

Ushiriki wa Benki Kuu katika Soko la fedha za kigeni unalenga katika kuleta utulivu wa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni pale ambapo kunakuwepo na mabadiliko yasiyokuwa ya kawaida katika soko. Mfumo huu umewezesha kuwepo kwa mabadiliko katika viwango vya kubadilisha fedha za kigeni yanayoendana na mabadiliko katika uchumi wa ndani na wa nje, hususan zile nchi ambazo tunafanya nazo biashara kwa wingi.

## UENDELEZAJI WA MASOKO YA FEDHA

Soko la fedha endelevu ni kigezo muhimu cha ufanisi wa sera ya fedha, utulivu wa sekta ya fedha na maendeleo ya uchumi. Kuanzishwa kwa masoko ya dhamana na minada ya fedha za kigeni miaka ya 1990 ilikuwa ni hatua za mwanzo ambazo Benki Kuu ilichukua katika kuendeleza shughuli za masoko ya fedha nchini. Kuanzishwa kwa masoko haya kumeiwezesha Serikali kukopa moja kwa moja kwa umma fedha za kuziba nakisi katika bajeti yake.

Minada ya fedha za kigeni ilianzishwa mwaka 1993 baada ya kupitishwa kwa sheria ya fedha za kigeni ya mwaka 1992. Mwaka 1994, soko la fedha za kigeni (Interbank Foreign Exchange Market, IFEM) lilianzishwa kuchukua nafasi ya minada ya fedha za kigeni. IFEM ni soko la jumla la fedha za kigeni linalohusisha benki na taasisi za fedha nchini. Soko hilo linatumika katika kuweka kiwango cha thamani ya shilingi ikilinganishwa na sarafu nyingine kubwa duniani. Ushiriki wa Benki Kuu katika soko hilo umelenga zaidi katika kutekeleza sera ya fedha na kuhakikisha utulivu wa soko hilo.

## CHANGAMOTO

Licha ya mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa sera ya fedha na maendeleo katika sekta ya fedha kwa ujumla, Benki Kuu imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile: uchumi kukabiliwa na misukosuko ya ndani na nje ya nchi, ufinyu wa zana za utekelezaji wa sera ya fedha, na ufinyu wa masoko ya fedha.

Vilevile, ukuaji wa sekta ya fedha unakwazwa na ukosefu wa mfumo wa kumbukumbu za wakopaji (credit reference system), kasi ya mabadiliko katika miundo na sheria za uendeshaji wa mabenki kitaifa na kimataifa ambayo inasababisha uhitaji wa taaluma na ujuzi wa hali ya juu na endelevu katika kazi ya usimamizi wa benki, mifumo dhaifu ya kufikisha malengo na matokeo ya zana za kutekeleza sera ya fedha hali ambayo kwa kiasi inadhoofisha viwango vya mafanikio malengo ya sera ya fedha, na mapungufu katika sheria mbalimbali ambazo husababisha benki kushindwa kutoa mikopo kwa sekta binafsi kwa kiwango cha kuridhisha.

## HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Ili kukabiliana na changamoto katika kutekeleza sera ya fedha, Benki Kuu itaendelea kufanya yafuatayo:

Kuboresha mipango na utekelezaji wa sera ya fedha itakayojumuisha uchambuzi wa masuala mbalimbali ya kiuchumi yanayoendana na sera ya fedha ili kuongeza mafanikio katika uchumi. Sanjari na hilo, Benki Kuu itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwepo wa mfumo wa ushindani katika masoko ya fedha ili kuongeza ufanisi na mchango wake katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya sera ya fedha na kukuza uchumi.

Kuendeleza ushirikiano na Serikali ili kuhakikisha sera ya fedha na ile ya mapato na matumizi ya Serikali zinawiana ili kuendeleza utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi.

Kujenga mfumo madhubuti wa malipo ili kuendeleza na kuimarisha utulivu katika sekta ya fedha pamoja na kuhimili changamoto zinazotokana na utandawazi na mabadiliko yanayotokea katika sekta ya fedha duniani.

Kushirikiana na wadau wengine kuboresha mazingira yatakayowezesha kujenga kwa mfumo utakaowezesha kukua kwa wigo wa huduma za kibenki kwa Watanzania walio wengi hasa wenye kipato cha chini ambao wanashindwa kupata huduma katika mfumo wa sasa. Benki imedhamiria kuimarisha sera ya kusimamia shughuli za utoaji wa mikopo midogo midogo (National Microfinance Policy).

Kusimamia utekelezaji wa awamu ya pili ya mageuzi katika sekta ya fedha (Second Generation Financial Sector Reforms) yanayolenga kuongeza mchango wa sekta ya fedha katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

**SERA YA MADENI**

Tangu Uhuru uchumi wa Tanzania umepitia vipindi tofauti vilivyoathiri Sera za Madeni ya Taifa. Vipindi hivyo ni; Miaka ya Mwanzo ya Uhuru (1961-1966), Kipindi cha Uchumi Dola (1967-1985) na Kipindi cha Maboresho ya Kiuchumi (1986-mpaka sasa).

**MIAKA YA MWANZO YA UHURU (1961-1966)**

**a. Deni la ndani**
Ukopaji ulifuata Sheria ya Mikopo ya Ndani kama ilivyorekebishwa mwaka 1961 (Local Loans (Amendment) Ordinance 1961) iliyotaka mikopo kutozidi paundi milioni nane katika mwaka husika. Bado Tanzania ilikuwa chini ya Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki (East African Currency Board) na hivyo ukopaji wa ndani kutokidhi mahitaji kwa kuwa uwekezaji wa Bodi ya Sarafu katika hatifungani za Serikali haukutakiwa kuzidi asilimia 17 ya uwekezaji wake wote.

**b. Deni la nje**
Ukopaji ulifanywa kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo na Dhamana ya mwaka 1962 (Loans and Guarantees Act, 1962) iliyozuia ukopaji unaozidi paundi milioni 20 au kiwango chochote zaidi kitakachoidhinishwa na bunge kwa mwaka husika. Katika miaka ya 1960, Serikali ilikopa kiasi kikubwa kutoka nchi wahisani, kilichotumika kwa ajili ya maendeleo hususan katika eneo la usafirishaji lililopewa asilimia 52 ya mikopo yote.

## KIPINDI CHA UCHUMI DOLA (1967-1985)

### a. Deni la ndani na nje

Mwaka 1966, Tanzania ilianzisha Benki Kuu na hivyo kupunguza vizingiti vya ukopaji wa ndani. Vilevile, sera ya Ujamaa na Kujitegemea ilisababisha kutaifishwa kwa benki za biashara na hivyo kusaidia ukopaji wa Serikali kutoka vyanzo vya ndani. Mwaka 1974, Serikali iliidhinisha Sheria mpya ya Mikopo, Madeni, Dhamana na Misaada (the Government Loans Guarantee and Grants Act, 1974), iliyotaka mkopo mpya (wa ndani au nje) uwe hausababishi gharama za ulipaji wa deni lote la Serikali katika mwaka wa fedha husika na miaka minne inayofuatia kuzidi asilimia 30 ya wastani wa mapato ya kila mwaka ya Serikali. Aidha, kwa ukopaji wa nje sheria mpya ya mwaka 1974 ilielekeza mkopo mpya uidhinishwe kama hausababishi gharama za ulipaji wa mikopo yote ya nje katika mwaka wa fedha husika na miaka minne inayofuatia kuzidi asilimia 15 ya wastani wa mapato ya fedha za kigeni ya kila mwaka.

### b. Changamoto za Kiuchumi na Kisiasa.

Katika kipindi hiki, changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia (1974 na 1979) na kuyumba kwa bei ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi, Kusambaratika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 kulikosababisha kuundwa mashirika mapya ya umma kama reli, bandari, ndege, na Vita ya kumng'oa Nduli Idd Amin mwaka 1978-1979, zilijitokeza na kufanya Deni la Taifa lianze kukua kwa kasi.

## KIPINDI CHA KUBORESHA UCHUMI (1986-2011)

Ili kuhakikisha kuwa Deni la Taifa linaendelea kuhimilika pamoja na changamoto zilizojitokeza, jitihada kadhaa zilichukuliwa na Serikali kama:

Kufanya mazungumzo na wakopeshaji ili kuleta unafuu wa madeni. Namna mbalimbali zilitumika kama kufuta madeni na kuongeza muda wa madeni kuiva (debt cancellation and debt rescheduling), kubadili madeni kuwa misaada. Jitihada hizi zilisaidia kupata msamaha wa madeni mengi katika kipindi cha 2001-2006 kutoka Nchi Wahisani na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa chini ya utaratibu wa HIPC na MDRI.

Kufanya mabadiliko ya kisheria yatakayoendana na mazingira mapya. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ilifanyiwa marekebisho mwaka 2003 ambapo pamoja na kuendelea kuwepo kwa masharti ya mwaka 1974, sheria mpya inaitaka Serikali ikope mikopo yenye unafuu (grant element) isiyo chini ya asilimia 35. Sheria hii imeunda Kamati za Usimamizi Madeni (Debt Management Committees) na kuainisha mgawanyo na majukumu ya kitaasisi katika usimamizi wa madeni ya Serikali. Vile vile sheria nyingine mpya kama za; Huduma za Kibenki na Taasisi za Kifedha, Masoko na Mitaji, na Benki Kuu ziliidhinishwa ili kuleta ufanisi katika ukopaji wa ndani.

Kuandaa mikakati mipya itakayotoa mwongozo wa wapi Serikali ikope. Serikali iliandaA Mkakati wa Deni la Taifa la Nje (Externa Debt Strategy) mwaka 1999, na Mkakati wa Deni la Taifa wa mwaka 2002 (National Debt Strategy) ambapo Serikali imetakiwa kukopa kutoka vyanzo nafuu vya Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Vilevile, katika mwaka fedha 2010/11, Serikali iliandaa Mkakati wa Kusimamia Deni la Taifa kwa Muda wa Kati (Medium Term Debt Management Strategy). Mpango huu umeainisha na kukokotoa gharama na athari za kila aina ya mikopo ambayo Serikali inatarajia kukopa na hivyo kushauri aina bora ya mikopo ili Deni la Taifa liendelee kuhimilika.

Kufanya Tathimini ya Ustahilimivu wa Deni la Taifa (National Debt Sustainability Analysis) kila baada ya Miaka miwili. Kutokana na mafanikio makubwa katika tasnia ya uchumi mpana, tathmini ya hivi karibuni (mwaka 2010), inaonesha kuwa Deni la Taifa linahimilika, na hivyo kuashiria uwepo na utekelezaji wa sera nzuri zinazotia matumaini.

**HALI ILIVYO SASA**

Deni la ndani linajumuisha Dhamana za Serikali zinazouzika na zisizouzika katika masoko ya fedha. Hii inatokana na kuanzisha dhamana za muda mfupi (Treasury bills) mwaka 1993 na Dhamana za muda mrefu (Treasury bonds) (miaka 2 mwaka 1993 na miaka 5, 6, 7 na 10 mwaka 2002).Dhamana za muda mfupi (siku 35 na 91) ni kwa ajili ya kudhibiti ujazi wa fedha na siyo matumizi ya Serikali. Kwa dhamana zinazouzika tangu mwaka 1997, Serikali imekuwa ikiziuza upya pale zinapoiva (rollover).

Deni la nje kwa kiasi kikubwa linatokana na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa kwa mujibu wa sheria na mikakati iliyopo sasa. Hata hivyo, kutokana na vyanzo vya Mashirika ya Fedha ya kimataifa kutotosheleza mahitaji makubwa ya shughuli za maendeleo na kwa kuzingatia kuwa deni la Serikali bado linahimilika, katika mwaka wa fedha 2010/11, Serikali iliamua kuanza kukopa kutoka katika vyanzo vya kibiashara kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Mazungumzo na vyanzo hivyo yamefanikiwa na Serikali imeshaanza kupata fedha hizo.

## 9.2 SHERIA

Sheria zilizotungwa chini ya Wizara ya Fedha au zilizotungwa na Taasisi zilizochini ya Wizara ya Fedha ni kama ifuatavyo;

**Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura Na. 418 ya Mwaka 1959**

Sheria ya Msajili wa Hazina ilitungwa na kupitishwa mwaka 1959 ili kusimamia rasilimali na hisa za Serikali kwa niaba ya Rais katika Mashirika na Taasisi za Umma ambapo Serikali imewekeza.

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 2002 na kuitwa Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina (Powers and Functions) Sura Na. 370. Aidha, mnamo mwezi Aprili, 2010 Sheria hii ilifanyiwa marekebisho yaliyosababisha kuundwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina inayojitegemea.

**Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania**

Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1965 na kufanyiwa marekebisho mnamo mwaka 1978, ili kuipa Benki Kuu uwezo wa kukabiliana na mabadiliko na changamoto zilizojitokeza katika kusimamia mabadiliko ya uchumi vijijini, viwanda na ongezeko la mahitaji ya fedha za kigeni.

Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995 ilipitishwa ili kuiwezesha Benki Kuu kuondokana na majukumu mengi na kuiwezesha kujikita katika majukumu makuu ya usimamizi wa utulivu wa bei (Price Stability) na utekelezaji wa sera ya fedha inayozingatia misingi ya soko huria.

Sheria mpya ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006 (Bank of Tanzania Act) ilianzishwa ili kuwezesha, pamoja na mambo mengine, kuimarisha Benki Kuu kuiwezesha

kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na mabadiliko katika sekta ya fedha duniani.

**Sheria ya Fedha za Umma, Sura Na.348**

Sheria ya Fedha za Umma, Sura Na. 348 ndio Sheria mama ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Kunapotokea mgongano wa Sheria hii na Sheria zingine kuhusu masuala ya fedha, Sheria hii Sura Na.348 ndio inayopaswa kufuatwa (Prevail).

Sheria ya Fedha za Umma, Sura Na. 348 ilianzishwa na Bunge mwaka 1961, Wakati huo ikijulikana kama the Exchequer and Audit Ordinance, 1961. Sheria hii imeendelea kutumika hadi mwaka 2001 ilipofutwa na kutungwa Sheria mpya iliyojulikana kama the Public Finance Act, Sura Na. 348. Sheria hii ndio inayotumika hadi sasa.

Madhumuni ya Sheria hii ni pamoja na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali kwa kutoa Miongozo, Kanuni na Taratibu za masuala yote ya fedha yanayohusu utunzaji wa fedha, uandaaji wa taarifa za fedha na kutunza kumbukumbu za fedha.

Kuanzishwa kwa Sheria hii kumeimarisha zaidi suala la usimamizi wa fedha za umma katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya maeneo hayo ni kama ifuatavyo: Kuanzishwa kwa mfumo wa malipo (IFMS); Kuanzishwa kwa Idara ya Internal Auditor General chini ya Wizara fedha; Kutoa taarifa za fedha zilizo sahihi na kwa wakati; Wizara ya Fedha kuwa na uwezo wa kusimamia fedha za Umma katika Serikali za Mitaa; Kuongezeka kwa nidhamu katika matumizi ya fedha za umma.

## Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 (The Public Procurement Act, Cap.410)

Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura Na. 410 inasimamia masuala yote ya ununuzi wa umma. Sheria hii ilianzishwa mwaka 2001. Kabla ya Sheria hii kutungwa, Serikali ilikuwa inatumia Kanuni za ununuzi zilizokuwa zikijulikana kama Financial Orders Part III- Stores Regulations. Kanuni hizi zilianzishwa mwaka 1961.

Sheria ya Ununuzi wa Umma ilitungwa mwaka 2001. Aidha, Sheria hii ya mwaka 2001 ilifutwa na kutungwa Sheria nyingine ya Ununuzi wa Umma Mwaka 2004, kufuatia uboreshaji uliopendekezwa mwaka 2002.

Katika kutekeleza Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni na miongozo mbalimbali imeandaliwa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Sheria hiyo.

## Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya Mwaka 1994 Sura Na. 79 ndiyo Sheria mama inayoratibu na kusimamia Masoko ya Mitaji na Dhamana hapa Tanzania. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ndiyo Taasisi inayosimamia utekelezaji wa Sheria hii.

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 1997 na kuruhusu uwekezaji wa pamoja katika vikundi (Collective Investment Schemes) ili kuwawezesha Watanzania kukuza mitaji yao kwa haraka zaidi na kwa pamoja. Marekebisho hayo pia yameainisha namna ya utoaji au uuzaji wa Hisa katika Soko la Awali (Initial Public Offer) pamoja na masuala ya matangazo yahusuyo Hisa na Dhamana kwa wawekezaji.

Marekebisho mengine ni ya mwaka 2010 ambayo yametambua pamoja na mambo mengine, uwepo wa soko la pili kwa ajili ya Kampuni ndogo na za kati pamoja na Wataalamuu wapya wajulikanao kama Mshauri Mteule (Nominated Advisor). Sheria hii pia iliweka kipengele kuwezesha uundwaji wa Baraza la Masoko ya Mitaji na Dhamana (Capital Market and Securities Tribunal) kama msuluhishi wa mwisho wa migogoro inayoibuka katika Soko la Hisa, imeongeza nguvu za kisheria kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imetambua masuala ya ushirikiano wa Kimataifa kati ya Mamlaka na Mashirika ya Kimataifa na kuongeza makali ya faini kwa makosa mbalimbali yaliyoainishwa katika Sheria hiyo.

Zaidi ya marekebisho ya mwaka 2010 Mamlaka kwa sasa inafanya mapitio ya sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa malengo ya kushughulikia upungufu huo.

### Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Watumishi wa Umma

Sheria Na. 2 ya Mafao ya Hitimishio la Kazi kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 (Cap. 371) ilianzishwa ili kuchukua nafasi ya Sheria ya Pensheni Sura Na. 381 ya mwaka 1954 (Pensions Ordinance Cap. 371 of 1954) ambayo ndiyo ilikuwa ikitumika kulipa mafao kwa watumishi wa Serikali Kuu wanapofikia ukomo wa utumishi wao. Kwa mujibu wa Sheria hiyo Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma ulianza rasmi shughuli zake tarehe 1 Julai 1999.

Aidha, Sheria hii imepitia mabadiliko mbalimbali kuhusiana na malipo ya mafao kwa watumishi wa Serikali Kuu. Hii ni pamoja na mabadiliko madogo ambayo yalihusisha kubadilishwa kwa vifungu vya sheria na mabadiliko

makubwa ambayo yalihusisha kufutwa kwa sheria ya zamani (yaani Pension Ordinance ya mwaka 1954) na kuanza kwa sheria mpya (yaani Sheria Na. 2 ya Mwaka 1999).

**Sheria ya Bima**

Sheria ya Bima Sura Na. 18 ya mwaka 1996 ilitungwa ili kusimamia na kuratibu shughuli za Bima nchini. Mnamo mwaka 2002, Sheria hii ilifanyiwa marekebisho na kuwa Sheria ya Bima Sura Na. 394 ya mwaka 2002, ambayo ilitumika kwa kipindi cha miaka kumi (1996-2007) na kubainika kwamba haikidhi matakwa ya soko la bima na kanuni za Kimataifa zinazoongoza soko la bima. Hivyo, mwaka 2009 Sheria hiyo ilifutwa na kutungwa Sheria nyingine Na. 10 ya mwaka 2009 ambayo ilianzisha Mamlaka ya Bima nchini.

**Sheria iliyoanzisha Benki ya Posta**

Benki ya Posta Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 11 ya mwaka 1991 iliyofanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Bunge Na.11 ya mwaka 1992. Benki ya Posta ilianza shughuli zake rasmi tarehe 1 Machi, 1992 kutoka kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania ambalo lilirithishwa kutoka Tanganyika Post Office Savings Bank (TPOSB) ambayo iliundwa kwa Sheria ya mwaka 1925 na kuanza rasmi 1927.

**Sheria ya Rufaa za Kodi**

Bodi ya Rufaa za Kodi imeanzishwa kwa Sheria ya Rufaa za Kodi ya mwaka 2000 Sura Na. 408 kwa lengo la kushughulikia migogoro yote ya kodi inayotokea baina ya mlipakodi na Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA). Kabla ya kuundwa kwa chombo hiki malalamiko na migogoro ya kodi ilikuwa ikishughulikiwa na Mahakama pamoja na chombo

kilichokuwa kikiitwa National Tax Appeals Board (NTAB) ambacho kilishughulikia malalamiko ya Kodi ya Mapato (Income Tax) peke yake. Tofauti na ilivyokuwa awali Bodi ya Rufaa za Kodi inashughulikia migogoro ya kodi za aina zote, inayotokana na sheria zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Sheria ya Rufaa za Kodi (Tax Revenue Appeals Act Cap. 408) imekuwa ikifanyiwa marekebisho madogo madogo mwaka 2004-2006, lakini mwaka 2007 kumekuwa na marekebisho makubwa katika sheria husika na yaliyosababisha kurekebishwa kwa kanuni zake "Tax Revenue Appeals Board Rules, 2001" mnamo mwaka 2009.

Aidha, Baraza la Rufaa za Kodi limeanzishwa kwa sheria ya Rufaa za Kodi ya mwaka 2000 (Tax Revenue Appeals Act Cap. 408) kwa lengo la kushughulikia migogoro yote ya kodi inayotokana na uamuzi wa Bodi ya Rufaa za Kodi kwa haraka. Kabla ya kuundwa kwa chombo hiki malalamiko na migogoro ya kodi ilikuwa ikishughulikiwa na mahakama pamoja na chombo kilichokuwa kikiitwa National Tax Appeals Board (NTAB) ambacho kilishughulikia malalamiko ya Kodi ya Mapato (Income Tax) peke yake, upande wowote ambao haukuridhika na Uamuzi huo, rufaa zilikuwa zikiwasilishwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Baada ya hapo rufaa zilikwenda Mahakama ya Rufani Tanzania yenye mamlaka ya mwisho. Kwasasa, baraza linashuhulikia migogoro inayotokana na aina zote za kodi ambazo sheria zake zinasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**Sheria iliyoanzisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997, (The Executive Agencies Act 1997) (Act No. 30 of 1997).

Aidha, mwaka 2000 NBS ilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 125 la mwaka 2000. Kabla ya hapo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilikuwa ni Idara Kuu ya Takwimu chini ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango. Idara ya Takwimu ilikuwa inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Na. 33 Sura ya 443 ya mwaka 1961.

**Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania**

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzishwa chini ya Kifungu (4) cha Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura 399 (Kama ilivyorekebishwa mwaka 2006). Sheria hiyo ilianza kutumika mnamo tarehe 7/8/1995 kwa tangazo la Gazeti la Serikali Na. 419/1995.

Sheria zilizorithiwa na Mamlaka ya Mapato kutoka idara za kodi chini ya Hazina ni kama ifuatavyo: Sheria ya Kodi ya Mapato 1973, Sheria ya utozaji Kodi ya Forodha 1976, Sheria ya Usimamizi wa shughuli za Forodha 1970, Sheria ya Kodi ya Mauzo 1976, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sheria ya Ushuru wa Stempu, 1972, Sheria ya Ushuru wa Barabara, 1985, Sheria ya Ushuru wa Hoteli, 1972, Sheria ya Matumizi ya Magari 1911, Sheria ya Ushuru wa Viwanja vya Ndege 1962, Sheria ya Usajili na Sihia ya Magari 1972, Sheria ya Ushuru wa Bandari 1973, Sheria ya Usalama Barabarani 1973, Kodi ya Majengo 1985, Sheria ya Forodha na Ushuru 1977, Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa 1970, na Sheria ya maridhiano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 1987.

Kodi ya mauzo ilifutwa ilipofika tarehe 1/7/1998 na kuanzishwa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Mnamo mwaka 2004, sheria mpya ya kodi ya mapato, 2004 sura 332 ilianza kutumika. Aidha sheria ya usimamizi wa shughuli za forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2004 ilipitishwa na kuanza kutumika tarehe 1/1/2005.

**Sheria iliyoanzisha Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT)**

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilianzishwa tarehe 19 Juni, 2003, chini ya Sheria ya Bodi ya Wadhamini Sura Na. 318. Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilianzishwa kama mrithi wa taasisi ambayo hapo awali ilijulikana kwa jina la Dhamana ya Ubinafsishaji kwa Sheria ya Bunge iliyotungwa mwaka 1997.

**Sheria Iliyoanzisha Chuo Cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP)**

Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma kilianzishwa rasmi kama taasisi chini ya sheria ya Bunge Na. 8 ya mwaka 1980. Sheria hiyo ilianzisha chuo kisheria kikiwa ni kituo muhimu cha taifa cha kutoa mafunzo, kufanya utafiti, na kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika mipango ya maendeleo vijijini.

**Sheria iliyoanzisha Shirika Hodhi la Serikali (CHC)**

Shirika Hodhi la Serikali (CHC) lilianzishwa kwa jina la NBC Holding Corporation (NBCHC) kwa mujibu wa sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1997 kutokana na uamuzi wa Serikali wa kuivunja na kuirekebisha iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara iliyoundwa kwa Sheria Na 1 ya mwaka 1967. Shirika lilianza kutekeleza majukumu yake tarehe 1 Oktoba 1997 likiwa na kipindi cha miaka mitano kukamilisha shughuli zake.

**Sheria Iliyoanzisha Taasisi Uhasibu Arusha**

Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA) ilianzishwa kwa sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 1 ya mwaka 1990.

## 10.0 MABADILIKO NA MATUKIO MAKUU KATIKA MFUMO WA KIUCHUMI

Serikali ya Tanzania tangu ipate Uhuru mwaka 1961, imekuwa ikikabiliana na maadui wakuu watatu wa maendeleo ambao ni Ujinga, Maradhi na Umaskini. Maadui hao ambao waliathiri uchumi wa nchi kabla na baada ya Uhuru.

Mipango mbalimbali ya Maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu ilikuwa ikibuniwa katika kukabiliana na umaskini na kukuza uchumi. Mipango hiyo imeendelea kuboresha kipato, upatikanaji wa elimu, afya na huduma nyiginezo za kijamii. Sanjari na mipango hiyo, Tanzania iliandaa dira mbalimbali za maendeleo kwa lengo la kupunguza umaskini na kukuza uchumi. Miongoni mwa dira hizo ni:

**Azimio la Arusha la Mwaka 1967**, lilifafanua falsafa ya ukombozi wa kiuchumi na kijamii chini ya misingi ya Ujamaa na Kujitegemea kama lengo la muda mrefu kwa Watanzania. Hivyo, kuanzia Februari 1967 Dira ya Maendeleo ya Taifa sawia na Sera za Mageuzi ya kijamii na Kiuchumi ziliongozwa kwa misingi ya Azimio la Arusha.

**Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025** ilianza kutekelezwa mwaka 1995, na ndiyo inayoongoza harakati za maendeleo ya uchumi na jamii kufikia 2025. Madhumuni

ya Dira hii ni kuamsha, kuunganisha na kuelekeza juhudi na fikra zetu na rasilimali za Taifa letu katika maeneo ya msingi yatakayowezesha kufikia malengo ya maendeleo.

**Mkakati wa Kitaifa wa Kuondoa Umaskini (National Poverty Eradication Strategy (NPES).** Mkakati huo ulikuwa na malengo ya kupunguza umaskini kufikia 2010, ulitoa dira kuhusu umaskini na uboreshaji wa maisha ya jamii. Madhumuni yake yalikuwa ni kutoa mwongozo kwa wadau wote katika kutambua, kutekeleza na kutathmini hali ya umaskini. Mkakati ulitafsiri malengo yake katika maeneo ya ukuaji wa uchumi, kipato, elimu ya msingi, upatikanaji wa maji, magonjwa, afya na vifo, ajira, makazi na miundombinu, kuratibu sera na programu kwa muda mfupi na mrefu. Changamoto iliyojitokeza katika Mkakati huu ni kwamba ingawa uliundwa chini ya mfumo shirikishi, ulishindwa kuweka bayana vipaumbele miongoni mwa mipango yake ya utekelezaji na kuifanya kutofaa kama mpango kazi.

**Mkakati wa Misaada Tanzania 'Tanzania Assistance Strategy' – (TAS)** huu ulikuwa ni mkakati wa muda mfupi wa kitaifa wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii uliojumuisha mikakati ya Serikali na ya kimataifa katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi. Mkakati huu ni matokeo ya majadiliano kati ya serikali ya Tanzania na washirika wa maendeleo kuhusu misaada kwa Watanzania katika kutekeleza agenda za maendeleo ambapo masuala ya misaada kwa Tanzania yalijadiliwa mara kwa mara na kufanyiwa tathmini.

**Mkakati wa Kupunguza Umaskini 'Poverty Reduction Strategy Paper' (PRSP 2000 – 2003).** Mkakati huu ulilenga zaidi katika kuondoa umaskini ingawa katika utekelezaji wake ulikumbwa na changamoto za ufinyu wa bajeti.

**Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA).** Katika jitihada za kukuza uchumi na kuondoa umaskini na kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Serikali iliandaa na inaendelea kutekeleza mkakati huu. MKUKUTA ni mwendelezo wa mikakati ya kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Awamu ya kwanza ya MKUKUTA iliandaliwa mwaka 2004 na kupitishwa na Bunge Februari 2005 na utekelezaji wake kuanza rasmi katika mwaka wa fedha 2005/06 utekelezaji wake ulikuwa wa miaka mitano yaani 2005 – 2010; MKUKUTA wa kwanza ulitekelezwa kupitia nguzo kuu tatu ambazo ni ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini wa Kipato, Maisha Bora na Ustawi wa Jamii, Utawala bora na Uwajibikaji. Awamu ya pili ya MKUKUTA imeanza mwaka 2011/12

## 11.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA TANGU WAKATI WA KUPATA UHURU MWAKA HADI SASA (1961- 2011)

Tangu Uhuru jitihada mbalimbali za kupunguza umaskini zimeanza kuleta mafanikio. Hali ya maisha ya Watanzania ilivyo leo sivyo ilivyokuwa wakati tunapata Uhuru. Watu wengi zaidi sasa, wanapata elimu, huduma za afya, maji, na miundombinu ya barabara imeboreshwa. Serikali inao uwezo mkubwa zaidi wa kuwahudumia wananchi wake kuliko ilivyokuwa kabla ya uhuru. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

### 11.1 Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato.

#### Uchumi kwa Jumla

Uchumi wa Tanzania umeonesha mafanikio ya kuvutia tangu uhuru,ingawa mdororo wa uchumi na fedha duniani uliathiri maendeleo ya ukuaji wa sekta binafsi

kutokana na kupungua kwa mikopo iliyokuwa ikitolewa kwa sekta hiyo na kupungua kwa mapato yatokanayo na usafirishaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Mfano, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, Uchumi wa Tanzania umeonesha kukua kwa takribani wastani wa asilimia 7 ya Ukuaji wa Pato la Ndani (GDP)

Ukusanyaji wa mapato umeongezeka kutokana na mabadiliko ya sera na kuboresha taasisi. Katika mwaka 2007/08 kwa mfano, Serikali ilifanya marekebisho ya viwango vya kodi na taratibu za ukusanyaji wa mapato. Uwiano wa Mapato na Pato la Ndani umeongezeka kutoka asilimia 12 mwaka 2005/06 mpaka kufikia asilimia 16 mwaka 2009/10.

**Hali ya Umaskini wa Kipato**

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya kwa Tanzania Bara uliofanyika mwaka 2007 unaonesha kuwa kati ya mwaka 2001 na 2007, Umaskini umepungua kwa kiasi kidogo. Kiwango cha jumla cha umaskini kilipungua kwa asilimia 2.2 kutoka asilimia 35.6 mwaka 2000/01 hadi asilimia 33.4 mwaka 2007. Kiwango cha kupungua kwa umaskini ni kikubwa zaidi katika maeneo ya mijini ikilinganishwa na maeneo ya vijijini. Katika Jiji la Dar-es-Salaam, Umaskini ulipungua kutoka asilimia 17.6 mwaka 2000/01 hadi asilimia 16.2 mwaka 2007. Maeneo mengine ya miji umaskini ulipungua kutoka asilimia 25.8 mwaka 2000/01 hadi asilimia 24.1 mwaka 2007, wakati ambapo umaskini katika maeneo ya vijijini ulipungua kutoka asilimia 38.7 mwaka 2000/01 hadi asilimia 37.4 mwaka 2007. Kwa ujumla, kiwango cha umaskini kimepungua kwa asilimia 5 katika kipindi cha mwaka 1991/92 hadi 2007.

**Jedwali Na. 4**

**Hali ya Umaskini Tanzania Bara**

| Kuwepo kwa umaskini | | Maeneo | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mwaka wa Utafiti** | **Dar es Salaam** | **Maeneo mengine ya mijini** | **Maeneo ya vijijini** | **Tanzania Bara** |
| Chakula | 1991/92 | 13.6 | 15 | 23.1 | 21.6 |
| | 2000/01 | 7.5 | 13.2 | 20.4 | 18.7 |
| | 2007 | 6.7 | 12.9 | 18.4 | 16.5 |
| Mahitaji muhimu | 1991/92 | 28.1 | 28.7 | 40.8 | 38.6 |
| | 2000/01 | 17.6 | 25.8 | 38.7 | 35.6 |
| | 2007 | 16.2 | 24.1 | 37.4 | 33.4 |

**Chanzo:** Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya - 1991/92, 2000/01, na 2007

## 11.2 Sekta za Kukuza Uchumi

### Sekta ya Viwanda

Sekta ya viwanda nchini inaendelea kukua na kuchangia katika Pato la Taifa. Viwanda vyetu kwa sasa vinazalisha bidhaa zenye ubora unaokidhi viwango vya masoko ya ndani na ya nje. Kuna mafanikio makubwa katika kuongeza thamani katika sekta ya viwanda, sekta hii bado ina changamoto zinazojitokeza ikiwemo jamii kutopenda bidhaa zinazozalishwa nchini. Juhudi zaidi zinaendelea kufanyika ili kuweza kufikia ukuaji angalau wa asilimia 15 ifikapo mwaka 2015.

## Sekta ya Kilimo

Tangu uhuru 1961 Tanzania imekuwa na mikakati mbalimbali katika kuboresha kilimo kama vile Ukulima wa kisasa, Vijiji vya Ujamaa, Siasa ni Kilimo, Chakula ni Uhai, na Kilimo cha Kufa na Kupona. Ili kupunguza japo nusu ya umaskini wa chini ya dola moja kwa siku kufikia mwaka 2015 lengo ni kukuza kilimo kwa asilimia 10 kwa mwaka tofauti na asilimia 3.3 ya sasa.

Ili kufikia malengo hayo Serikali imeongeza kasi ya mapinduzi ya kilimo kwa kuzindua **KILIMO KWANZA** ambayo inajumuisha sera na mikakati inayolenga katika kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili kilimo kutumia fursa nyingi zilizopo.

KILIMO KWANZA ni muhimili muhimu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na inaweka msukumo zaidi katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Tofauti na mikakati iliyopita ambayo ilikuwa inapangwa na kutekelezwa na Serikali na taasisi zake, KILIMO KWANZA ni ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Katika ubia huu sekta binafsi ni wakala wa utekelezaji wa KILIMO KWANZA.

## Sekta ya Madini

Sekta ya madini inachangia takribani asilimia 2.3 ya Pato la Taifa, ambayo inakadiriwa kufikia asilimai 10 ifikapo 2025. Madini ni sehemu muhimu inayoongoza katika pato la kigeni kati ya mauzo yasiyo asilia. Aidha ina uwezo mkubwa wa ajira na inaongoza katika kuupa nguvu uchumi wa Tanzania. Kumekuwa na mabadiliko makubwa katika sekta hii tangu uhuru, Pato la Taifa kupitia madini limeongezeka kutokana na ubinafsishaji ambapo Serikali imekuwa ikikusanya kodi na kuchangia katika Pato la Taifa.

## Sekta ya Barabara

Maeneo mengi vijijini sasa yanafikika kwa barabara. Kwa mfano, mtandao wa barabara nchini umepanuliwa hadi kufikia kilomita 85,000. Changamoto iliyopo ni kuzifanya barabara zipitike wakati wote. Barabara za lami zimeongezeka kutoka kilometa 1300 zilizokuwapo mwaka 1961 hadi kufikia kilomita 5,626 hivi sasa kati ya barabara zenye urefu wa Kilometa 12,809 za Barabara Kuu Nchini.

Sekta ya barabara kwa miaka kadhaa sasa imepewa kipaumbele kama ilivyo katika utekelezaji wa Programu ya Uwekezaji katika sekta ya Usafirishaji (TSIP). Uwiano wa barabara zilizo katika hali nzuri na za wastani umeongezeka hadi kufikia asilimia 89 mwaka 2010.

## Sekta ya Nishati

Serikali iliendelea kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Nishati na Upanuzi wa Upatikanaji wa Nishati (TEDAP) ili kuboresha upatikanaji na ugavi wa umeme. Jumla ya Gigawati 3,290.25 kwa saa za umeme kutoka katika uzalishaji wa nguvu ya maji zilizalishwa ikilinganishwa na Gigawati 2,917.03 kwa saa mwaka 2008. Hii ni sawa na nyongeza ya asilimia 12.8 ambayo inatokana na uzalishaji wa umeme kutoka katika gesi asilia. Serikali pia inaendelea kupeleka na kusambaza umeme katika Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya na Vijiji mbalimbali.

Baadhi ya Miradi inayoendelea kutekelezwa hivi sasa ni ile inayogharamiwa na Mfuko wa Changamoto na Milenia (Millenium Challenge Account), JICA, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Serikali kupitia Wakala wa Umeme vijijini, inatayarisha Mkakati Kabambe wa kupeleka umeme Vijijini na kuimarisha Mfuko wa Nishati Vijijini. Lengo ni kukamilisha upelekaji wa Umeme kwenye Mikoa na Wilaya ambako Gridi ya Taifa haijafika na kujipanga vizuri katika kuongeza kasi ya kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na kuondoa umaskini, hasa katika maeneo ya Vijijini kwa kuwapelekea umeme hatua kwa hatua.

## 11.3 Maisha Bora na Ustawi wa Jamii

Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kuboresha utoaji wa huduma za kijamii, hususan elimu, afya, maji, udhibiti wa usafi wa mazingira na juhudi za hifadhi za jamii.

### Elimu

Kumekuwa na programu mbalimbali za kuendeleza sekta ya elimu. Juhudi mbalimbali kwa ajili ya kuboresha utoaji wa elimu katika ngazi zote zimeendelea kufanyika na mafanikio yamepatikana ikilinganishwa na hali iliyokuwepo wakati uhuru unapatikana.

Kwa sasa kuna shule za msingi 15,816 zenye wanafunzi 8,419,305 ikilinganishwa na shule 3000 zilizokuwepo baada ya uhuru ambazo zilikuwa na wanafunzi 486,000 tu.

Aidha, nchi ilikuwa na shule za sekondari 54 na Seminari 9 tu zote zikiwa na jumla ya wanafunzi 13,897. Hivi sasa tunazo Shule za Sekondari 4,237 katika Kata 3,338 hapa Nchini. Wakati wa Uhuru kulikuwa na Wanafunzi 11,832 wa Sekondari na hadi kufikia mwaka 2010 kulikuwa na Wanafunzi 1,638,699, sawa na ongezeko la asilimia 13,850.

Nia ni kuendelea kuongeza shule za sekondari ili kila kata nchini iwe na angalau sekondari moja. Wakati wa Uhuru kilikuwepo chuo kikuu Kimoja. Sasa hivi kuna jumla ya vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki 32 nchini.

## Afya

Wakati tunapata uhuru huduma za afya zilikuwa duni na hazikutosheleza mahitaji ya watu. Watu wengi waliishi kwa kutegemea mitishamba na waganga wa asili. Mafanikio mengi yamepatikana kwenye sekta ya afya tangu uhuru mpaka sasa.

Lengo la serikali ni kuwa na zahanati moja kila Kijiji. Zahanati zilizopo hivi sasa ni 4,717 nchi nzima. Dhamira ya serikali ni kujenga Vituo vya Afya katika kila Kata. Hadi sasa tunavyo Vituo vya Afya 534. Aidha, kati ya Wilaya 114 zilizopo kwa sasa, tunazo hospitali za Wilaya 57. Wilaya ambazo hazina hospitali, Serikali imeweka utaratibu wa kuwa na Hospitali Teule ambazo hadi sasa zipo 18.

Mikoa karibu yote ina Hospitali za Mikoa (isipokuwa katika Mikoa mipya). Kuna Hospitali za Rufaa Kanda ya Kaskazini (KCMC), Kanda ya Ziwa (Bugando) na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Hospitali ya Rufaa ya Mbeya). Kanda ya Kusini na Kanda ya Kati bado hazina hospitali za rufaa na juhudi za kujenga zinaendelea. Vilevile, Serikali ilijenga hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambayo ina Vitengo mbalimbali muhimu vinavyotoa huduma kwa Wananchi.

**Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

Utaratibu mzima wa urasimishaji unajumuisha shughuli za Upimaji wa Vijiji, Utoaji Hati miliki za Kimila, Upimaji wa Viwanja Mijini na Utoaji Hatimiliki.

**Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA)**

Serikali ilianzisha mpango huu kwa madhumuni ya kuboresha mazingira ya biashara nchini na kuboresha huduma zitolewazo na Serikali ili kusaidia Sekta binafsi ifanye kazi kwa ufanisi zaidi.

## 11.6 Mifuko ya Uwezeshaji

Kuanzia miaka ya 1990, kumeanzishwa mifuko mbalimbali inayosaidia katika kuinua hali ya wananchi kiuchumi. Mifuko hii imekuwa na mafanikio makubwa licha ya changamoto mbalimbali zinazoikabili ili kuhudumia Wananchi kwa wingi. Mifuko hii ni pamoja na:-

**Mfuko wa Wanawake (Women Development Fund-WDF)**

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kuwapatia wanawake mikopo yenye masharti nafuu. Mfuko huu unasimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Hadi kufikia mwaka 2000 Mfuko ulikuwa umekopesha jumla ya shilingi 648, 071,635, na marejesho yalikuwa shilingi 217, 646,164 (33.6%).

Mafanikio yaliyotokana na mfuko huu ni pamoja na kujenga nyumba bora; Kulipa ada za shule za watoto wao; Kujenga

nidhamu ya matumizi ya fedha; Kuhamasisha vikundi vya wanawake kujiunga na SACCOS; na kuzirahisishia Halmashauri ufuatiliaji wa marejesho ya fedha zilizopitishiwa SACCOS.

**Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF)**

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1993/4 kwa lengo la kutoa mikopo midogo yenye masharti nafuu kwa Vijana ili kuanzisha na kuimarisha miradi ya maendeleo. Hadi kufikia 2007/08 fedha za Mfuko huo zilizokuwa zimetolewa ni shilingi 2, 872, 770,000.

Mafanikio ya Mfuko ni pamoja na kusogezwa kwa huduma za mfuko kwenye Halmashauri za Manispaa, Wilaya na Miji kote Tanzania. Pia vijana wameweza kuanzisha miradi endelevu; na mfuko umejenga dhana chanya ya ukopaji.

**Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wanawake katika Sekta isiyo Rasmi**

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2000, chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa wakati huo kwa lengo la kuwawezesha wanawake kuanzisha na kuendeleza ajira binafsi kupitia miradi midogo, kuwaondoa katika ajira hatarishi, kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, kuwawezesha kuanzisha vikundi na kujiunga kwenye SACCOS, kuimarisha SACCOS zilizoanzishwa baada ya mradi kukua na kuunda shirikisho la SACCOS zao. Aidha, mpaka sasa Wanawake wapatao 2000 wa kipato cha chini na Vijana wapatao 500 walioibuliwa katika mazingira hatarishi, wamenufaika na Mfuko huu.

## Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo ya Nje (ECGS)

Mfuko wa udhamini wa mikopo kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi ulianza mwaka 2002/2003 kwa lengo la kutoa udhamini kwa benki za biashara ili ziweze kutoa mikopo kwa wauza bidhaa nje, ikijumuisha wakulima, wafanyabiashara na vyama vya ushirika. Mfuko huu ulilenga Biashara ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi na miradi mikubwa ya uwekezaji. Hadi kufikia Oktoba 2008, mtaji wa mfuko ulikuwa shilingi 30,514,687,335 na ulitoa udhamini wa Shilingi 272,955,353,233 wakati jumla ya mikopo iliyotolewa ni Shilingi 361,982,595,481.

## Mfuko wa Kudhamini Benki na Taasisi za Fedha kwa Ajili ya Kuboresha Utoaji wa Mikopo kwa Miradi Midogo na ya Kati (SME – CGS)

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2005/06 chini ya Benki Kuu ya Tanzania. Lengo la Mfuko huu ni kukuza na kuendeleza miradi midogo na ya kati (SMEs) ya wajasiriamali kwa kuwapa uwezo wa kifedha na mtaji ili kuboresha kipato chao, kuinua hali zao za maisha, na kuongeza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa. Walengwa wa Mfuko huu ni wajasiriamali Watanzania. Mfuko umeongeza mitaji kutoka shilingi milioni 500 (2005) hadi shilingi bilioni 5.751 Machi, 2010.

## Mfuko wa Maendeleo ya Wafanyabiashara Wananchi (NEDF)

Mfuko wa NEDF ulianzishwa kwa lengo la kuwapatia mitaji wajasiriamali wadogo wakiwemo wa sekta isiyo rasmi ili kuongeza uzalishaji. Kiwango cha juu cha mkopo kiliongezwa kutoka shilingi 500,000 kwa mwombaji hadi kufikia shilingi milioni 2.5 kwa miradi ya uzalishaji. Hadi kufikia Juni, 2008 jumla ya mikopo iliyotolewa ni shilingi

15,175,339,000 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kuwafikia wajasiriamali wapatao 36,178 tu. Katika robo ya kwanza 2009/10, jumla ya mikopo 1,450 yenye thamani ya shilingi 925,800,000 iliidhinishwa na kutolewa.

**Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF)**

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1994 kwa Sheria ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (The Agricultural Inputs Trust Fund Act No. 9 of 1994), kwa lengo la kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa waagizaji na wasambazaji wa pembejeo kwa mkulima mmoja mmoja, vikundi pamoja na shughuli zote za kuboresha hali ya upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo.

Hadi kufikia mwaka 2008/09, Serikali ilikwishatoa jumla ya shilingi 24,751,781,493 na marejesho yalikuwa shilingi 14,606,598,385 (59%).

Serikali ilifanikiwa kuongeza fedha katika mfuko wa pembejeo kutoka shilingi bilioni 4.9 hadi shilingi bilioni 30.1. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 16.3 zilitumika kuagiza matrekta na jumla ya matrekta 3,948 yameingizwa nchini katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010.

**Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)**

Mfuko huu ulianzishwa na Serikali mwaka 1984, kwa kusudio la kufanya kiwe chombo huru kinachojitegemea hapo baadaye. Mfuko iliandikishwa chini ya Trustee Incorporation Ordinance of 1956, chapter 375 of Tanzania Laws. Mwaka 1998 Mfuko iliandikishwa kama Taasisi Ndogo ya Fedha – NGO na kuruhusiwa kufanya shughuli zake nchini. Kiasi cha shilingi 4,812,735,000 zimeshatolewa na kuwafikia wadau wapatao 61,345.

## Mfuko wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo (Small Entrepreneurs Loan Facility - SELF)

Mfuko huu ulianza mwaka 2000 na madhumuni yake ni kuwawezesha Watanzania kupata mitaji, hususan walioko vijijini. Shughuli zake ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kupitia asasi za kifedha, kujenga uwezo wa asasi za kifedha, kujenga uwezo wa wajasiriamali waliopata mikopo na kuhamasisha wadau mbalimbali kuhusu shughuli za SELF.

Mafanikio ya mfuko huu yanaonyesha mikopo iliyotolewa kupitia SELF iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 5.6 mwaka 2005 hadi Shilingi bilioni 25.1 mwezi Machi 2010 sawa na ongezeko la asilimia 348. Taasisi za fedha zilizonufaika na SELF ziliongezeka kutoka 175 mwaka 2005 hadi 247 Machi 2010 sawa na ongezeko la Taasisi 72. Idadi ya Wananchi wanaonufaika na mikopo hiyo imeongezeka kutoka 20,526 mwaka 2005 hadi 69,795 mwaka 2010.

Kiwango cha urejeshaji mikopo ni kizuri (95%) na walengwa wameelewa umuhimu wa mikopo kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Wakopaji wengi wamekuwa wakiitumia mikopo yao vizuri katika kuboresha shughuli zao za kiuchumi.

## Mradi wa Kusaidia katika Shughuli za Kuongeza Kipato "Support to Income Generating Activities" katika Mikoa ya Pwani na Kigoma.

Katika mchakato wa kupunguza umaskini Tanzania, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji kupitia Shirika la BTC, zimekubaliana kutekeleza mradi wa miaka mitatu kuanzia Juni 2009 – 2012. Walengwa wa mradi huu ni wajasiriamali wadogo wanaoishi vijijini na mijini, Wanawake wajasiriamali, vijana wajasiriamali wenye umri kati ya miaka 15-25 na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Lengo Kuu la mradi huu ni Kuchangia katika Kuboresha Maisha ya wananchi hasa vijijini. Mradi huu unaratibiwa na Wizara ya Fedha na kutekelezwa na Halmashauri husika ambazo zilichaguliwa kwa kigezo cha kuwa na kiwango kikubwa cha umaskini nchini ambazo ni Rufiji, Mkuranga na Mafia katika Mkoa wa Pwani na Kigoma vijijini, Kibondo na Manispaa ya Kigoma katika Mkoa wa Kigoma.

Mafanikio ya mradi huu ni pamoja na kuongezeka kwa uwezo wa walengwa wa mradi kuhitaji na kupata huduma za kiufundi, ujasiriamali na biashara; Kuboresha uwezo wa watoa huduma zinazohusiana na biashara katika kufuata/kuhusianisha mahitaji ya walengwa wa mradi na kuboresha uwezo wa Halmashauri katika kuwezesha maendeleo ya kiuchumi.

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF)**

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) uliundwa na Serikali kama moja ya programu za kuziwezesha jamii zenye kipato cha chini kuinua hali ya maisha yao kwa kuanzisha shughuli zitakazoinua uchumi wao kupitia taasisi zao wenyewe.

Katika awamu ya kwanza (2000 –2005) jumla ya miradi 1,704 ilipitishwa na kupewa fedha. Miradi iliyokamilishwa ni 1,365

Awamu ya pili (2005 – 2009) jumla ya miradi 9,012 iliibuliwa na jamii katika Halmashauri zote nchini. Miradi iliyopatiwa fedha ni 7,546 yenye thamani ya Shilingi bilioni 156. Miradi 4,078 kati ya hiyo imekamilika na kukabidhiwa kwa Wananchi na sasa imeanza kutoa huduma kwa wananchi. Jumla ya vikundi 1,720 vya kuweka akiba vyenye wanachama 21,712, vimeundwa. Vikundi 1,000 vimepewa vifaa vya kutunzia akiba vikiwemo sefu na vitabu vya kumbukumbu.

## Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira kwa Kutoa Mikopo yenye Masharti Nafuu (Mabilioni ya J. K.)

Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali ilianzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi maarufu kama "Mabilioni ya JK" kwa ajili ya kuwakopesha Wajasiriamali wadogo. Hadi kufikia mwezi Mei 2010, jumla ya Shilingi bilioni 47.1 za awamu zote mbili zilikwishakopeshwa kwa Wajasiriamali na Vikundi mbalimbali katika Mikoa yote na kunufaisha Wajasiriamali zaidi ya 72,000.

## Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi (MEF)

Ili kuwawezesha wananchi kupata mitaji na mikopo Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004 Kifungu cha 16(1) inaagiza kuanzishwa kwa Mfuko wa uwezeshaji " Mwananchi Empowerment Fund" unaosimamiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Aidha, Mfuko huu ni kichocheo cha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kukuza uelewa wa kuwekeza miongoni mwa Watanzania; Kuongeza ajira; Kuwa kiunganishi kati ya taasisi, Kampuni na mashirika yaliyosajiliwa chini ya Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuratibu shughuli zao na kutoa ushauri na kuyaendeleza; na kukopesha fedha kwa vikundi vya wananchi, SACCOS, watu binafsi, Mashirika na Taasisi kwa njia ya dhamana au bila dhamana.

## 11.7 UANZISHWAJI WA TAASISI ZA UWEZESHAJI ZA SERIKALI

### Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)

Baraza la Taifa la Uwezeshaji liliundwa mwaka 2005 na kuanza kazi yake rasmi mwezi Mei, 2007 kwa kupewa dhamana ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughulizi zote za Uwezeshaji Wananchi Kitaifa. Baraza lina majukumu makuu manne kama yalivyoainishwa katika Sheria Na.16 ya mwaka 2004. Majukumu hayo ni pamoja kuwajengea Watanzania uwezo wa kushiriki katika shughuli za Kiuchumi; Kushawishi na kuhamasisha uwekaji wa akiba, uwekezaji na kushiriki kikamilifu katika uchumi; Kuhamasisha na kusaidia biashara za ushirikiano zinazoongozwa na Watanzania; na kusimamia, kuratibu na kutafuta vyanzo vya fedha na michango kwa ajili ya mfuko wa uwezeshaji.

Aidha, Baraza limepewa jukumu la kusimamia Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuongeza ajira kwa kutoa Mikopo yenye masharti nafuu.

### Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje

Kuanzia mwaka 2006 hadi 2008, jumla ya viwanda 46 vimesajiliwa chini ya Mpango wa EPZ, vikiwemo viwanda 18 vya kujenga miundombinu ya EPZA na viwanda 28 ni vya uzalishaji. Mamlaka ya EPZ imeanza kuhamasisha Wawekezaji kwa kujenga viwanda katika eneo la Benjamini William Mkapa - SEZ (BWM-SEZ) Mabibo, DSM na tayari Wawekezaji 24 wamewasilisha maombi ya kuwekeza katika eneo hilo. Wawekezaji 5 wamepewa leseni na kujenga viwanda katika eneo hilo.

## 12.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA TANGU UHURU MWAKA 1961

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni;

a. Namna ya kuongeza mapato ya ndani kwa kupanua wigo wa kodi ili kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nje,

b. Kuwa na uchumi unaokuwa kwa kasi kubwa sanjari na ongezeko la idadi ya watu,

c. Namna ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni,

d. Kuongeza fursa za ajira na kuwanufaisha wananchi walio wengi hasa vijana ambao ndio kundi kubwa katika soko la ajira,

e. Kuimarisha sekta ya fedha ili wananchi wengi hasa wanaoishi vijijini waweze kupata huduma za kibenki na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo vijijini,

f. Namna ya kushirikisha sekta binafsi katika uchumi pamoja na sekta isiyo rasmi ili ziweze kuchangia katika mapato ya Serikali.

## 13.0 MATARAJIO YA WIZARA YA FEDHA KATIKA MIAKA 50 IJAYO

### Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Miaka Hamsini ijayo nchi inatarajiwa iwe na uchumi ulioimarika, asilimia kubwa ya wananchi wake kuwa wenye uwezo wa kumiliki uchumi wa nchi yao pamoja na kuwa na

tabaka kubwa la wananchi lililo la kati (middle class). Hii ni pamoja na:

a. Kuimarika kwa programu za Uwezeshaji na kuweza kuwafikia na kuwanufaisha wananchi walio wengi;

b. Kuhakikisha kwamba nguzo za uwezeshaji zinaleta tija kwa wananchi;

c. Kuendelea kujenga uchumi wa nchi na Taifa linalojitegemea; Kuwawezesha wananchi kiuchumi ili waweze kumiliki uchumi wa nchi kwa asilimia 80;

d. Kuendelea kujenga uchumi wa nchi ili kumudu ushindani katika mazingira ya utandawazi na kuongeza tija;

e. Kuendeleza juhudi za kuwezesha wananchi kiuchumi ili waweze kumudu fursa za kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa nchi na hatimaye kuleta mapinduzi ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda;

f. Kuwa na Taifa lenye sauti ya kukabili uchumi wa Soko la Dunia, mabadiliko ya utandawazi na nguvu za kiuchumi, na

g. Kuendelea kujenga na kuboresha mazingira mazuri ya Sekta binafsi na kuongezeka kwa mchango wake katika Pato la Taifa.

## 13.1 Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

Katika kuhakikisha uchumi wetu unakua na umaskini wa kipato unapungua, matarajio ya baadaye ya Serikali ni kama ifuatavyo:

a. Kuwa na vyanzo mbalimbali vya uzalishaji na uchumi wenye maendeleo ya viwanda yaliyo sawa na nchi zenye mapato ya kati;

b. Kuwa na uchumi wenye kasi ndogo ya mfumuko wa bei na uwiano madhubuti wa uchumi kwa jumla;

c. Kuwa na ukuaji wa uchumi kwa asilima 8 au zaidi kwa mwaka; Kuwepo na miundombinu ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji;

d. Kuwa mshiriki na mshindani shupavu katika masoko ya nje na kupanga na kuendeleza maslahi ya nchi na kuwa na uwezo wa kujirekebisha haraka ili kuweza kukabili mabadiliko yanayotokea katika masoko ya nje; na

e. Kuwa na ukuaji wa uchumi unakwenda sawia na urekebishaji wa hali ya sasa ya uharibifu wa mazingira na rasilimali kama vile misitu, samaki, vyanzo vya maji, hali ya hewa, udongo na viumbe hai mbalimbali.

## 13.2 Maisha Bora na Ustawi wa Jamii

Ili kuwa na maisha bora na ustawi wa jamii kwa Watanzania kwa kutumia mikakati na sera zilizopo, Serikali imelenga kufikia malengo yafuatayo:

a. Kujitosheleza kwa chakula na kuwa na uhakika wa upatikanaji wake muda wote;
b. Elimu ya msingi kuwafikia wote, kufuta ujinga na kufikia kiwango kinachoridhisha cha elimu ya kati na juu kulingana na mahitaji ya kuwa na watendaji wenye uwezo wa kushughulikia kikamilifu changamoto za kimaendeleo katika ngazi zote;

c. Kufikia usawa wa kijinsia na kuwapa fursa wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni; Upatikanaji wa huduma za msingi kwa watu wote;

d. Upatikanaji wa huduma bora za uzazi kwa watu wote wenye umri unaostahili; Kupunguza vifo vya watoto wachanga na vifo vinavyotokana na uzazi kwa robo tatu ya viwango vya sasa;

e. Upatikanaji wa maji safi na salama kwa watu wote;

f. Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati; na

g. Kuondoa kabisa umaskini uliokithiri.

## 13.3 Utawala na Uwajibikaji

Katika utawala bora na uwajibikaji Serikali inatarajia kufikia malengo ya kuwa na jamii yenye sifa zifuatazo;

a. Maadili mema na kuthamini utamaduni, Uadilifu na kuheshimu Utawala wa Sheria,

b. Kutokuwepo rushwa na maovu mengine, na

c. Jamii iliyoelimika, inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu, na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake.

## 13.4 Kuratibu na Kusimamia Upatikanaji wa Misaada na Mikopo (Kupunguza Utegemezi wa Misaada Kutoka Nje)

Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa misaada na mikopo kulingana na Mkakati wa Pamoja wa

Misaada Tanzania (MPAMITA). Kila mwaka Serikali imekuwa ikipokea misaada kupitia utaratibu wa Misaada ya Bajeti (GBS), Mfuko wa pamoja (Basket Fund) na Misaada ya Miradi ya Maendeleo. Katika vikao vinavyofanyika kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, Serikali imekuwa ikisisitiza kupatiwa misaada mikubwa zaidi katika utaratibu wa GBS.

Manufaa ya utaratibu wa GBS ni mengi ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

a. Kuhakikisha fedha zinaingia kwenye Mfuko Mkuu na matumizi yake kuidhinishwa na Bunge;

b. Kuipa Serikali uwezo zaidi wa kuongoza katika mchakato wa maendeleo ya nchi;

c. Kuruhusu ugawaji wa fedha za maendeleo kwa nchi nzima kufuatana na vipaumbele;

d. Kuelekeza misaada ya kiufundi/ushauri wa kitaalamu kwa kuzingatia matakwa ya nchi; na

e. Kusaidia kupunguza gharama za majadiliano na maelewano kati ya Serikali na wadau wa maendeleo.

## 13.5 Kusimamia na Kudhibiti Deni la Taifa

Katika kutekeleza Mkakati wa Deni la Taifa, Serikali imeendelea kusimamia kwa umakini deni lake kwa kukopa zaidi kutoka vyanzo nafuu na kuchambua athari zinazotokana na mikopo mipya. Deni la Taifa lilikuwa asilimia 42.4 ya pato la taifa mwaka 2009/10 ikilinganishwa na asilimia 52.1 mwaka 2005/06. Vile vile uwiano wa deni la nje kwa pato la taifa ulipungua kutoka asilimia 38.5 mwaka 2005/06 hadi asilimia 22.5 mwaka 2009/10. Aidha, kutokana

na tathimini iliyofanyika katika robo ya kwanza ya 2010/11, ilionesha deni la Taifa linahimilika. Hii ina maana kuwa nchi yetu inakopesheka na kuweza kulipa deni bila kuathiri utengemavu wa uchumi.

### 13.6 Kusimamia na Kudhibiti Matumizi ya Serikali

Katika kuboresha usimamizi wa matumizi ya Serikali, Wizara ya Fedha itaendelea kutekeleza yafuatayo:

a. Kusambaza Mtandao wa Kompyuta wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha - IFMS kwenye Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Serikali za Mitaa. Hadi sasa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 86 pamoja na Balozi 7 tayari zinatumia mfumo huu. Wizara inaendelea na zoezi la kuweka mfumo wa IFMS kwenye Serikali za Mitaa na Balozi zetu zilizobaki;

b. Wizara kupitia Programu ya uboreshaji ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) itaendelea kujenga uwezo wa wafanyakazi hususan katika nyanja za usimamizi wa mapato na matumizi; na

c. Kupitia Kitengo cha ufuatiliaji wa matumizi ya Serikali, Wizara itaendelea kufanya uhakiki wa malipo ya mishahara ya watumishi, ufuatiliaji wa fedha za chakula cha wanafunzi katika shule za sekondari, ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa majengo na ukaguzi wa miradi ya barabara.

### 13.7 Usimamizi wa Vitega Uchumi vya Serikali

Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kusimamia Mashirika na Taasisi za umma ili zitekeleze majukumu yao kikamilifu na kuchangia katika mapato ya Serikali. Tathmini inafanyika kwa mashirika yaliyobinafsishwa na yale ambayo

yako katika mchakato wa kubinafsishwa ili kuhakikisha ustawi wenye tija wa Mashirika hayo. Aidha, Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370 ilirekebishwa ili kumpa Msajili wa Hazina mamlaka zaidi ya kusimamia ufanisi wa Mashirika na Taasisi za Umma.

## 13.8 Kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Wizara itaendelea kusimamia mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Majukumu hayo ni pamoja na:

Kutafuta wanachama, kukusanya michango kwa wakati, kuwekeza fedha za wanachama katika vitega uchumi vyenye tija na kulipa mafao ya wanachama kwa wakati. Hadi sasa mifuko hiyo imeendelea kufanya vizuri katika kufanikisha majukumu hayo.

Hata hivyo, zipo changamoto zinazoikabili mifuko ikiwa ni pamoja na

a. Kupanua wigo wa wanachama kwa kuongeza idadi yao,

b. Kuwekeza katika maeneo yanayohakikisha usalama wa fedha za wanachama na faida ya kutosha, na

c. Kuhakikisha uendelevu wa mifuko.

Kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeanza kazi mwezi Septemba, 2010 ni matarajio ya Wizara kwamba Mamlaka itaweza kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoikabili mifuko ya hifadhi ya jamii.

# (TUMETHUBUTU, TUMEWEZA NA TUNAZIDI KUSONGA MBELE)

Kimeandaliwa na

Wizara ya Fedha

S.L.P 9111, Dar es Salaam, Tanzania

+25522 2111174-6 | +25522 2110326